SUPA JACKPOT
TZS.1,104,580,144
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Vyuo** udereva 'janjajanja' kikaangoni

UKURASA 3


CAG alivyogonga hodi kwa Msajili, vyama vya siasa akikuta 'madudu'
Mapigano moto Sudan, jirani Kusini, Kenya na Djibouti wajitosa usuluhishi
siasa
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
Mkumbuke aliyekuwa Katibu Mkuu wa UN, pia Rais Dk. Kurt Waldheim
Uwekezaji wa Samia katika nguvukazi ya maelfu na ishara anakoelekeza nchi

UKURASA 11

Jumatano Aprili 19, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581285
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Walimu 240 walivyonaswa wakifundishwa 'ushetani'

- **Waliandaliwa** hoteli, posho kwa siku 10... *Ukurasa 2*




## ACT, polisi watibuana kisa Ripoti ya CAG

UK. 3




Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana wa ACT Wazalendo, Abdul Nondo akizungumza na waandishi wa habari, mbele ya askari polisi waliowawekea kizuizi cha ngao, ili wasifanye maandamano ya kuishinikiza serikali kuwachukulia hatua waliotuhumiwa kwa ubadhirifu wa fedha za umma kupitia ripoti ya CAG. Picha kushoto: Askari polisi wakizuia maandamano. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Muswada kubadili sheria umri kuoa, kuolewa waiva

UK. 2




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwa na viongozi mbalimbali na vijana walionufaika na programu KCB tujiajiri. Kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Anthony Msore, Mkurugenzi Mkazi wa GIZ, Dk. Mike Falke. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa KCB Group, Paul Russo, Mwenyekiti wa Bodi ya KCB Tanzania, John Ulanga, Kaimu Mkurugenzi wa Biashara wa Afrika Mashariki-KCB Group na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Cosmas Kimario. Ubia huo wenye thamani ya Sh. bilioni 2.2 utawezesha kuwainua vijana kiujuzi na kujiajiri kwenye sekta ya ujenzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**MICHEZO** VAR KUAMUA SIMBA VS WYDAD UK.24 **MAONI** UK.6



Mtaalam wa Ufungaji wa Bidhaa na Maboresho kutoka Kituo cha Kimataifa cha Biashara (ITC), Frederic Couty (aliyesimama), akifafanua jambo kwa wasafirishaji na wachakataji kutoka sekta ya ufugaji nyuki kuhusu vifaa vya ufungaji wa bidhaa, uwekaji nembo, miundombinu ya picha, barcode na usindikaji wa gharama nafuu, wakati wa mafunzo ya siku mbili, jijini Dar es Salaam juzi. Mafunzo hayo ni sehemu ya mradi wa kuboresha mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki (BEVAC) unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na kutekelezwa na ITC kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (Enabel). **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Walimu 240 walivyonaswa wakifundishwa 'ushetani'

**Na Mary Mosha,** SAME

KAMATI ya Usalama Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, imelazimika kuingilia kati na kusitisha mafunzo yaliyokuwa yanatolewa kwa walimu na taasisi isiyo ya kiserikali (jina tunalo) baada ya kubaini dosari, ikiwamo vitabu vinavyotumika kufundishia kuwa na viashiria vya maadili yasiyofaa.

Mafunzo hayo yalikuwa yanatolewa kwa walimu wa shule za msingi na sekondari wilayani humo, yakipewa jina la Mafunzo ya Afya ya Jamii, Afya ya Uzazi na Uhusiano.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Kasilda Mgeni alisema jana kuwa katika ufuatiliaji na vyombo vya usalama, wamebaini kuwapo upungufu mkubwa ikiwamo baadhi ya picha na maneno yaliyomo kwenye vitabu vilivyokuwa vinatumiwa na taasisi hiyo kufundishia kuwa na viashiria vya kuhamasisha mambo yasiyofaa kwa wanafunzi.

Alisema vitabu vilivyobainika kutumiwa na taasisi hiyo huenda ni miongoni mwa vilivyozuiwa na serikali kusambazwa na kutumiwa katika maeneo mbalimbali nchini hasa kwenye taasisi za elimu, kiongozi huyo akibainisha kuwa vitabu vyote vimechukuliwa kwa ajili ya uchunguzi zaidi, pia kufanyiwa marekebisho kabla ya kutumika kama itafaa.

"Tumefika katika eneo hilo, tumejionea wenyewe, picha na maneno yanayotumika kutoa mafunzo hayo hayafai kuwafundisha watoto wetu, hasa wa ngazi za msingi na sekondari, tumeyasitisha.

"Walimu wamefundishwa maadili na hiki wanachopata hapa hakiendani na maadili ya kitanzania na bado wanaendelea kusikiliza bila kukosoa, hili halikubaliki, ninaagiza vitatu hivi 246 vilivyokuwa tayari hapa vikusanywe, na mwalimu ataondoka yeye kama yeye, OCD vijana wako wanisaidie hiyo kazi sasa," Mkuu wa Wilaya aliagiza.

Alisema kamati yake ya ulinzi na usalama imemtaka mkurugenzi wa taasisi hiyo kusitisha shughuli zote zinazohusu mafunzo ya afya ya jamii, afya ya uzazi na uhusiano kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Same mpaka itakapoamuliwa vinginevyo, akimkata pia kusaidia vyombo vya usalama kutoa ufafanuzi wa masuala hayo.

**WALIVYONASWA**

Mwenyekiti wa Halmashauri wa Wilaya ya Same, Yusto Mapande alisema walioshiriki mafunzo hayo ni walimu wa malezi 244 kutoka shule za umma wilayani humo.

"Kila shule ilikuwa na mwakilishi mmoja ambaye wana mawasiliano yake. Mafunzo haya yalikuwa ni ya siku 10 na tumegundua hili siku ya tisa, tuligundua baada ya kuona magari yanatoka hotelini na kwenda eneo la mafunzo.

"Hawa walimu walipangiwa hoteli na kulikuwa na magari yalikuwa yanawachukua kupelekwa kwenye mafunzo na jioni wanarudishwa kwenye hoteli, walikuwa wanalipiwa kila kitu kikiwamo chakula na malazi," alisema.

Mwenyekiti huyo alibainisha kuwa kwa siku, walimu hao walikuwa wanalipwa posho ya Sh. 100,000. Hii ina maana kwamba, kila siku taasisi hiyo ilikuwa inatumia Sh. milioni 24 kwa ajili ya posho walimu hao na ingetumia Sh. milioni 244 kwa siku 10 zilizokuwa zimepangwa.

"Walichokuwa wanafundishwa ni kinyume cha utamaduni wa Mtanzania. Mafunzo haya yana kanzidata ya walimu wa kila shule wanaowapatia ambao moja ya kazi zao hapo baadaye ni kutoa mrejesho kwenye makundi yao ya WhatsApp na barua pepe," alibainisha.

Baadhi ya wazazi wilayani Same, akiwamo Saidi Mchomvu, waliiomba serikali kufanya misako na ukaguzi kwenye mashirika mbalimbli ya elimu ili kuwanusuru watoto dhidi ya 'ushetani' unaoukabili ulimwengu kutokana na mmomonyoko wa maadili.

"Wengine hatujafika shuleni, watoto wanafundishwa kwa lugha za kigeni, ni vigumu kubaini tatizo hilo mapema. Tunaomba viongozi wote kwa pamoja kuwekeza nguvu katika kuhakikisha wanatokomeza tatizo hilo," alisema Mwanahawa Athumani, mkazi wa Same.

# Muswada kubadili sheria umri kuoa, kuolewa waiva

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Katiba na Sheria imeliambia Bunge kuwa iko tayari kupeleka muswada bungeni wa marekebisho ya Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 ili kubainisha umri upi unafaa kuoa au kuolewa.

Waziri wake, Dk. Damas Ndumbaro alitoa kauli hiyo jana bungeni alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Thea Ntara aliyetaka kujua ni lini serikali itawasilisha marekebisho ya sheria hiyo.

Alisema Bunge liliagiza wizara ikusanye maoni ya wadau na mapendekezo, kazi ambayo imekamilika na sasa wako tayari kuwasilisha bungeni muswada wa marekebisho ya sheria hiyo.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali kuamua kuwa wasichana wasiolewe chini ya miaka 18.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis alisema Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, inatambua mtu mwenye umri chini ya miaka 18 kuwa ni mtoto, hivyo ni kosa la jinai kumhusisha na uhusiano ya kimapenzi, pia kumwozesha.

"Kwa upande mwingine, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inaruhusu mtoto wa kike kuingia kwenye ndoa akiwa na miaka 14. Hivyo, serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria imeshakusanya maoni kutoka kwa wadau kuhusu upi ni umri sahihi wa kuoa na kuolewa," alisema.

Alibainisha kuwa uchambuzi wa maoni hayo umeshakamilika na yatawasilishwa ndani ya Bunge ili yajadiliwe na mabadiliko kufanyika kadri Bunge litakavyoona inafaa ili kumlinda mtoto wa kike afikie ndoto zake.

Hayo yanafanyika huku kukiwa na uamuzi wa mahakama wa kurekebisha sheria, ili kutoruhusu watoto kuoa au kuolewa.

Oktoba 23, 2019, Mahakama ya Rufani ilitupa rufani ya serikali iliyokuwa inapinga hukumu ya Mahakama Kuu iliyobatilisha vifungu vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 vinavyoruhusu mtoto wa kike chini ya umri wa miaka 18 kuolewa.

Serikali ilikata rufani kupinga hukumu hiyo iliyotokana na kesi ya kikatiba iliyofunguliwa na mwanaharakati na Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Msichana Initiative, Rebeca Gyumi.

HABARI KITAIFA

# ACT, polisi watibuana kisa Ripoti ya CAG

Elizabeth Zaya na Halfan Chusi

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeingia katika mvutano na Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam baada ya vijana wa chama hicho kuitisha maandamano jana kushinikiza kuchukuliwa hatua watendaji wote waliohusika katika ubadhirifu wa fedha za umma.

Ubadhirifu huo ni uliotajwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kupitia ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 iliyowasilishwa bungeni Aprili 6 mwaka huu.

Mvutano huo uliibuka majira ya saa nne asubuhi baada ya askari wa jeshi hilo kufika makao makuu ya chama hicho Magomeni, Dar es Salaam kuzuia maandamano yaliyokuwa yamepangwa kufanywa na vijana hao.

Vijana hao ambao tayari walikuwa wamejipanga kwa ajili ya kuanza maandamano hayo, wakiwa wamebeba mabango yenye ujumbe mbalimbali ulioambana na nyimbo, walianza kusukumana na askari waliofika katika eneo hilo, huku kukiwa na majibizano baina yao.

Polisi walikuwa wakiwasukuma warudi ndani ya jengo la chama chao na kusitisha maandamano, huku vijana hao wakishinikiza kuendelea na mpango wao wa kufanya maandamano.

Askari hao walipofika katika eneo hilo, waliwaambia wasitishe maandamano hayo kwa madai kwamba tayari hatua zimeshaanza kuchukuliwa na mamlaka husika dhidi ya waliotajwa na CAG, hivyo hakukuwa na haja ya kuandamana.

Licha ya ufafanuzi huo, vijana hao walibaki na msimamo wao wakidai hatua stahiki zilizochukuliwa dhidi ya waliohusika na ubadhirifu wa fedha za umma kama ilivyoelezwa na CAG.

Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana ya ACT-Wazalendo, Abdul Nondo, baada ya kuzuiwa kufanya maandamano hayo, alisoma risala waliyokuwa wamepanga kumfikishia Rais Ikulu.

Nondo alisema kuwa Aprili 14 mwaka huu waliandika barua kwa Jeshi la Polisi kuomba kibali cha kufanya maandamano kutoka Manzese hadi Ikulu ya Dar es Salaam, lakini juzi jeshi hilo liliwajibu kwamba tayari Rais Samia Suluh Hassan ameshaanza kuifanyia kazi ripoti ya CAG, hivyo hakuna haja kufanya maandamano.

"Barua yenu imebeba maoni yenu kwamba mnaona hatua zimechukuliwa, lakini sisi ngome ya vijana wa ACT-Wazalendo tunaona kwamba bado hatua hazijachukuliwa na ndio maana leo (jana) tulitoa taarifa kwamba tutafanya maandamano ya amani kuonyesha hisia kwamba wabadhirifu wa nchi hii wanapaswa kuchukuliwa hatua," alisema Nondo huku polisi wakiwa wamesimama mbele yake.

Katika risala yao hiyo, Nondo alitaja wanayoshikiniza, yanajumuisha kuwataka baadhi ya watendaji, wakiwamo mawaziri, kujiuzulu nafasi zao kutokana na ubadhirifu uliofanywa na watendaji wa taasisi wanazozisimamia.

# Vyuo vya udereva wa ujanjaujanja kikaangoni

Na Ambrose Wantaigwa

MKUU wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Ramadhani Ng'anzi, amesema vyuo vyote vya kutoa mafunzo ya udereva nchini vitakaguliwa kuhakikisha visivyokuwa na vigezo vinafungiwa.

Alisema katika ukaguzi huo wataangalia uwezo na sifa za wakufunzi pamoja na mitaala kuhakikisha wanatoa mafunzo yanayowezesha kupatikana madereva wenye sifa kabla ya kupewa leseni.

Kamanda Ng'anzi alisema hayo alipozungumza na Nipashe kwamba katika ukaguzi huo vyuo vyote ambavyo vitakosa sifa na wakufunzi wasio na taaluma inayokidhi viwango vitafungwa.

Alisema hizo ni baadhi ya hatua za kikosi cha usalama barabarani kukabiliana na ongezeko la ajali nchini ikiwa ni pamoja na kufutwa dawati la utoaji leseni la kikosi hicho. Alibainisha chanzo kikuu cha ongezeko la ajali za barabarani nchini ni kutokana na baadhi ya madereva kukosa umahiri wakati wanapoendesha magari, wengine kutofuzu mafunzo yao vizuri katika vyuo vya udereva.

Alibainisha kwamba baadhi ya madereva wasio na sifa wanaendesha magari kwa mwendo kasi hali inayosababisha kushindwa kudhibiti vyombo vyao wakati ajali inapotokea.

Alisema kikosi hicho kimeanzisha uchunguzi kubaini madereva na vyuo vyote waliofanya udanganyifu na kusababisha kutolewa leseni kwa watu waliofeli mitihani ya ukaguzi ya udereva.

"Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Camilius Wambura aliagiza kikosi cha usalama barabarani wafanye uchunguzi ili kubaini wahusika wote wanaofanya udanganyifu wakati wa utoaji leseni ili wachukuliwe hatua zinazostahili," alisema Ng'azi.

Alisema uchunguzi unaendelea ikiwa ni pamoja na kubadilishwa watendaji katika dawati la utoaji leseni ili kuleta ufanisi katika utendaji wa kila siku wa kikosi hicho.

Kamanda Ng'anzi alisema kikosi hicho kimeanzisha matumizi ya teknolojia ikiwamo kufunga mitambo ya Kamera katika barabara kuu zote nchini baada ya kukamilika majaribio ya mitambo hiyo hivi karibuni.

"Hatua ya kuweka kamera za kisasa inatokana na baadhi ya askari wa usalama barabarani kuwa wachache nyakati za usiku na uwezo wa vifaa vinavyotumika sasa maarufu kama 'tochi' kushindwa kufanya kazi nyakati za usiku," alisema.

Alisema mfumo huo utawezesha kikosi hicho kufuatilia mwenendo wa madereva saa 24 nchi nzima na utakuwa na uwezo wa kubaini mwendo kasi na makosa mengine kama matumizi ya simu na kupita maeneo yasiyoruhusiwa.

Alikemea baadhi ya askari wa usalama barabarani kujihusisha na vitendo vya rushwa akisema yeyote atakayepatikana akichukua rushwa atachukuliwa hatua kali ikiwamo kufukuzwa kazi na kufikishwa mahakamani.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa kwa kikosi hicho juu ya tabia za baadhi ya madereva wanaokiuka sheria za usalama barabarani na kuongeza kwamba taarifa zao zitalindwa kwa ajili ya usalama wao.





MARK auctioneers

AUCTIONEERS AND COURT BROKERS COMPANY LIMITED

Our motto: Quality Services With Integrity

Head office Location: Kinondoni Mwanamboka
Contact: Mobile phone 0715884162/0754884162/0787884477
Email: inguku47@gmail.com
P.O. Box 72252
DAR ES SALAAM

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **AZANIA BANK LIMITED** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wake. Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea mahali ilipo dhamana.

| Na | JINA LA MDAIWA | MALI INAYOUZWA | MAHALI ILIPO MALI INAYOUZWA | SIKU NA TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | KIKUNDI CHA HAKIKA | KIWANJA AMBACHO HAKIJAENDELEZWA , KIWANJA KIPOKWA JINA LA EMMANUEL KASAWA RHOBI | KIPO KATA YA LAMADI WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU | IJUMAA TAREHE 5/05/2023 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI |
| | | NYUMBA YA KUISHI , IPO KWA JINA LA SARA AMISI MAGOMA | IPO KATA YA LAMADI WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU | IJUMAA TAREHE 5/05/2023 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI |
| | | NYUMBA YA KUISHI , IPO KWA JINA LA VERONICA SIMON MATHIAS | IPO KATA YA LAMADI WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU | IJUMAA TAREHE 5/05/2023 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI |
| | | PIKIPIKI YA MIGUU MITATU (TRICYCLE) YENYE NAMBA YA USAJILI MC 326 CUL YENYE KADI YA UMILIKI 8651031 . IKO KWA JINA LA EMMANUEL KASAWA RHOBI | IPO OFISI AZANIA BANK LIMITED TAWI LA LAMADI | IJUMAA TAREHE 5/05/2023 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI |
| | | NYUMBA YA KUISHI , IPO KWA JINA LA BIJA LAURENT BIJA | IPO KATA YA LAMADI WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU | JUMA MOSI TAREHE 6 /05/2023 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI |
| | | NYUMBA YA KUISHI , IPO KWA JINA LA ANECKY GILEADY MANGO | IPO KATA YA LAMADI WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU | JUMAMOSI TAREHE 6/05/2023 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI |
| | | NYUMBA YA KUISHI , IPO KWA JINA LA ALLEN SEIF JUMA | IPO KATA YA LAMADI WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU | JUMAMOSI TAREHE 6/05/2023 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI |
| | | NYUMBA YA KUISHI , IPO KWA JINA LA SALUMU NZANGIDA MADUHU | IPO ENEO LA ITONGO , KATA YA LAMADI , WILAYA YA BUSEGA , MKOA WA SIMIYU | JUMAMOSI TAREHE 6/05/2023 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI |
| 2 | FISH FARM GROUP B | NYUMBA YA KUISHI ILIYOPO KATIKA KIWANJA NA. 223, KITALU 'A'. NYUMBA IPO KWA JINA LA PROSPER JUBILET NDOSI | IPO ENEO LA MAJENGO MWANHUZI WILAYA YA MEATU MKOA WA SIMIYU | JUMA TANO TAREHE 10/05/2023 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA:-**

1. Mnada utafanyika sehemu ilipo dhamana.
2. Mnunuzi atakayefikia bei ya juu atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano 25% ya bei iliyofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano (75%) atalazimika kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya tarehe ya mnada.
3. Endapo mteja atashindwa kumalizia 75% ndani ya siku 14 kiasi kilichotolewa awali 25%i hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) pamoja na gharama nyingine ni juu mnunuzi.
5. Mali itauzwa kama ilivyo.

**Wote mnakaribishwa**

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-**

**Mkurugenzi Mtendaji,
Mark Auctioneers & Court Brokers Co Ltd
Court Brokers Co. Ltd,
P.O.Box 72252 , Dar es Salaam
Simu: 0754 884162/ 0768 897686/
0787 884477/0692 009805
Email: info@azaniabank.co.tz**

**Au**

**Mkurugenzi Mtendaji,
Azania Bank Ltd,
Mawasiliano Tower,
P.O. Box 32089,
Dar es Salaam.
Simu+255 22 2412025/6/7
Web: www.azaniabank.co.tz**

# Vyama vya siasa vyapendekeza taasisi za Hakijinai zifumuliwe

**Na Restuta James**

VYAMA vya siasa vimependekeza Taasisi za Hakijinai nchini zifumuliwe na kusukwa upya ili kuimarisha utoaji wa haki kwa usawa nchini.

Aidha, madereva bodaboda na bajaji, wamependekeza sheria iwabane madereva na abiria watakaotumia vyombo hivyo kinyume cha sheria.

Maoni hayo yalitolewa jijini Dar es Salaam jana viongozi wa baadhi ya vyama walipofika mbele ya Tume ya Kuangalia Namna ya Kuboresha Mifumo ya Taasisi za Hakijinai nchini, inayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu, Mohamed Othman Chande.

Mwanasheria wa Chama Cha Wananchi (CUF), Mashaka Ngole, alisema wamependekeza Mwendesha Mashtaka wa Serikali (DPP), awekewe mazingira ya kudhibiti matumizi ya kifungu kinachompa mamlaka ya kufuta kesi ili akifanya hivyo asiweze kumkamata tena mtuhumiwa.

Alisema wamependekeza kuwa DPP awe na mamlaka ya kufuta kesi na kufungua mpya katika hatua za awali na asiweze kumkamata mtuhumiwa kwa kesi ambayo ilishaanza kusikilizwa.

Kuhusu dhamana, Ngole alisema kwa kesi kubwa kama za mauaji na dawa za kulevya, kuwapo muda maalum wa upelelezi na ukiisha, mtuhumiwa apewe dhamana wakati upelelezi ukiendelea badala ya kumwacha mahabusu muda mrefu.

"Mtuhumiwa akikaa ndani mwaka mmoja basi apewe dhamana...sisi tunasema kuwe na namna ya kudhibiti hii mamlaka. Abaki nayo DPP kwa sababu yeye ndiye anayeanzisha kesi, lakini adhibitiwe na mahakama, pale atakapotaka kufuta kesi atoe taarifa na mahakama ipewe nafasi ya kusikiliza hiyo taarifa na ione uzito wa hiyo taarifa kabla ya kukubali kufuta kesi au vinginevyo," alisema.

"Atakapofuta kesi ambayo imeanza kusikilizwa, amemaliza mashahidi wake hiyo iwe mwisho wa mtuhumiwa kushtakiwa tena. Huu ni uchezeaji wa sheria afute kesi katika hatua za awali sio katika hatua za kusikiliza."

Kuhusu Polisi, Ngole alipendekeza kiundwe chombo mahsusi kitakacholiwajibisha jeshi la polisi pale askari wanapofanya kinyume cha sheria, kanuni na taratibu.

Alisema kumekuwa na malalamiko ya raia kunyanyaswa ndani ya vituo vya polisi na wakati mwingine kupoteza maisha katika mazingira ya kutatanisha, hivyo ni wakati wa kuundwa kwa chombo huru kitakachofanya uchunguzi.

Pia, alisema uwekwe utaratibu wa kupata fomu ya matibabu (PF-3), kwa raia atakayepigwa na kujeruhiwa na polisi na kwamba dhamana kwenye vituo vya polisi itolewe hadi siku za mapumziko.

Naye Makamu Mwenyekiti wa chama cha NRA Bara, Mohamed Majaliwa, alipendekeza kuwa maelezo ya awali ya mtuhumiwa yanayoandikwa polisi yarekodiwe au ahojiwe mbele ya kamera ili kuepuka ubambikiaji wa kesi.

"Kama mtuhumiwa anajua kusoma na kuandika aachwe aandike mwenyewe... masharti ya kuomba dhamana yawe ni rahisi na yanayotekelezeka," alisema.

Kuhusu Mahakama alisema kesi za rufani zimekuwa zikichukua muda mrefu kwa maelezo ya majaji kukosa bajeti ya vikao na kupendekeza kuwa uwekwe utaratibu wa kuzisikiliza kwa mishahara yao badala ya kutegemea posho.

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema: "Tunaona kuna uhitaji wa mageuzi makubwa ya ufumuaji wa mfumo wa kitaasisi, kisheria, kimwenendo katika taasisi zinazosimamia mfumo wa haki jinai."

Akizungumzia Jeshi la Polisi, Shaibu alisema linahitaji kufanyiwa mageuzi makubwa ya kimfumo, kimwenendo, kimafunzo na miundombinu ili lihudimie umma kwa ufanisi.

Kuhusu DPP, alisema sheria ibadilishwe ili iweke utaratibu mzuri wa kila mtuhumiwa mwenye haki ya kupata dhamana anaipata kwa DPP au polisi, wakati wowote na taasisi hizo zisipewe mamlaka ya kunyima dhamana.



Dereva wa bodaboda akipita kwenye mafuriko katika eneo la Ukonga Majumba Sita, jijini Dar es Salaam, yaliyosababishwa na mvua iliyonyesha jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Samia aagiza kutolewa kibali ajira wahandisi

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amesema Rais Samia Suluhu Hassan, ameelekeza kutolewa kwa kibali cha kuajiri watumishi 250 wa kada ya uhandisi.

"Lengo letu kubwa ni kuhakikisha watumishi hawa wapya wataweza kusimamia ujenzi wa miradi inayotekelezwa ili kuimarisha tawala zetu za mikoa lakini pia kuhakikisha tunakuwa na miradi ya maendeleo ambayo inakidhi vigezo," alitamka Waziri Angellah jana bungeni.

Alikuwa anajibu hoja za wabunge walichangia hotuba yake ya makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka ujao wa fedha, akibainisha kuwa kibali hicho kinahusisha wahandisi 100, wakadiriaji majenzi 100 na maofisa ununuzi 50.

Waziri alifafanua kwa kurejea katika serikali za mitaa kwamba hadi sasa kuna upungufu wa watumishi 1,773, unaowajumuisha maofisa watendaji kata, mitaa na vijiji.

Vilevile, Waziri Angellah alifafanua kuhusu hatima ya watumishi wanaojitolea katika maeneo mbalimbali ndani ya sekta ya afya na elimu kwamba, serikali inatambua kuwapo huduma zao katika mamlaka za serikali za mitaa, akitoa mfano umuhimu wa walimu katika shule za sekondari.

Alitoa angalizo kwamba hadi sasa serikali haina mfumo rasmi wa kutambua taarifa zao katika utumishi huo unaoendelea. Hata hivyo, unaandaliwa utaratibu mahusus wa kutumia mifumo ya kielektroniki kupitia wizara mama za taaluma hizo ili wahusika hao watakapoomba ajira rasmi, taarifa zao ziwapo.

"Hivyo basi, kwa sababu hii, baadhi ya walimu na hasa katika sekta ya afya wamekuwa wakipata nafasi za kujitolea. Kweli, lakini wako wengine walitamani wazipate pia, hawajawahi kuzipata nafasi hizi na wamekuwa wakipata nafasi katika shule, lakini vilevile katika vituo vya kutolea huduma za afya.

"Kukosekana kwa mfumo au utaratibu huo ulio rasmi na ulio wazi, bado unaweka ombwe kati ya walimu wanajitolea na watumishi wengine wa sekta ya afya," alisema.

Vilevile, alieleza katika halmashauri, mchakato unaendelea wa kununua magari ya wagonjwa (ambulance) 528 kuondoa pengo la hitaji, kila hamashauri inatarajiwa kupata magari walau mawili.

# Mvua yaharibu nyumba, mali

**Na Waandishi Wetu**

ZAIDI ya nyumba 30 yakiwemo majengo ya kanisa na Shule ya Rubafu sambamba na mali mbalimbali za wananchi, vimeharibiwa na mvua kubwa iliyoambatana na dhoruba kali na radi iliyonyesha katika Kijiji cha Marehe, Bukoba mkoani Kagera.

Mvua hiyo iliyoanza kunyesha majira ya usiku wa kuamkia juzi imesababisha madhara kwa kuharibu mali pamoja na makazi ya kambi ya wavuvi wa mwalo wa Mahele huku watu wawili wakihofiwa kufa maji kutokana na dhoruba hiyo.

Wakisimulia tukio hilo juzi, baadhi ya wakazi wa kijiji hicho walisema mvua hiyo ilinyesha wakati wamelala na walishtuka na kukuta tayari baadhi ya nyumba zimewaangukia ndipo walipoanza juhudi za kuokoana.

Gordian Lurian, mkazi wa kijiji hicho, alisema takriban nyumba 32 zimeezuliwa, hivyo kufanya wananchi wa eneo hilo kukosa makazi. Pia alisema jengo jipya la Kanisa Katoliki lililojengwa miezi mitano iliyopita liliezuliwa na mvua hiyo.

"Baada ya kushtuka tulikuta baadhi ya watu tayari wamefika kwa ajili ya kusaidia kuokoa watu waliongukiwa na nyumba hususani watoto kwa kuvunja milango na kuwaondoa ndani," alisema Godliver Rweyemamu, mkazi wa kijiji cha Marehe.

Justine Mchunguzi, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Rubafu, alisema madhara ya mvua katika shule hiyo alisema mapaa mawili yaliezuliwa na kusababisha kuharibika kwa mabati na makenchi kwenye madarasa hayo.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Rubafu alisema katika tukio hilo watu wawili ambao walikuwa wakiendelea na uvuvi wa samaki katika Ziwa Victoria, wanahofiwa kufa maji baada ya kutokuonekana tangu dhoruba hiyo ilipotokea.

Akizungumza baada ya kutembelea waathirika hao, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Erasto Sima, alisema juhudi za kuwapata wavuvi hao wawili zinaendelea na watafuatilia katika kijiji alipopatikana mwenzao ili kuona uwezekano wa kuwapata na wao pia.

Katika hatua nyingine, Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Pwani, Mhandisi Baraka Mwambage, amesema hatari katika eneo lililokuwa limemomonyoka kwa mvua la Kimange Barabara ya Chalinze –Segera, kwa sasa imeondoka.

Mwambage amesema eneo hilo lilibomolewa na mvua kubwa iliyonyesha April 15, mwaka huu. Mita nne na nusu kwenda chini ilimomong'olewa mita moja na nusu iliachwa kwa njia ya kutoka Dar es Salam na kufanya watumiaji kutokuwa salama huku upande wa kutoka Tanga ukiwa salama.

Akitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliyetembelea kukagua barabara hiyo juzi, alisema tayari eneo lililoathiriwa na mvua hizo limejengwa kwa mawe na zege kutoka chini na kazi hiyo ilikamilika juzi.

Kwa mujibu wa Mhandisi Mwambage, baada ya hatua hiyo kukamilika eneo hilo litaachwa kwa siku saba ili mchanganyiko wa zege na mawe ukomae na kuwezesha kubeba mzigo wa magari.

**Imeandaliwa na Vitus Audax, MWANZA, na Julieth Mkireri, PWANI.**

TANGAZO


A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
KILIMANJARO
DRINKING WATER
FURAHIA MAISHA
NA MAJI ASILIA
500ml
1000ml
1500ml
6L
12L
18.9L
+255 659 536 937, +255 758 979 641, +255 659 785 276
kdw@bbl.co.tz
kilimanjarodrinkingwater
kilimanjaro_drinking_water

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maofisa benki wapewe elimu kuhudumia wenye ulemavu mikopo

**SHIRIKISHO** la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), limelalamikia taasisi za fedha zinazobeba dhamana ya kutoa mikopo kuhusu elimu duni kwa maofisa wake na kusababisha kundi la watu wenye ulemavu kutopewa kipaumbele wanapohitaji mikopo benki.

Kundi hilo limedai baadhi ya benki kuwanyanyapaa, kutokana na maofisa wake kutokuwa na elimu ya kuwasaidia watu hao na haki zao katika kupata huduma bora zenye usahihi kwa kundi hilo.

Kundi hilo limebeba watu wenye ulemavu wa aina mbali mbali, kuna wengine wasioona, wasiosikia (viziwi) na wasioweza kuongoea (bubu), hivyo ni lazima wafikiriwe kwa kupatiwa huduma sahihi kulingana na ulemavu wao.

Katibu Mkuu wa SHIVYAWATA, Jonas Lubago, anasema katika Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022, iliyowasilishwa bungeni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, alisema amebaini mamlaka 180 za serikali za mitaa hazikukusanya mikopo.

Mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ya Sh. bilioni 88.42 haikukusanywa kutokana na kutokuwapo kwa ujuzi wa kutosha kwenye Idara ya Maendeleo ya Jamii. Idara hiyo ngazi ya mamlaka ya serikali ya mitaa haikuwa na ujuzi wa kutosha kufanya upembuzi yakinifu kwa vikundi vilivyoomba mikopo, kuvisimamia katika kufanya urejeshaji wa mikopo na kutoa mafunzo ya biashara kwa wanufaika.

"Kati ya kiasi hicho Sh. bilioni 2.25 zinahusu vikundi vilivyoacha shughuli za biashara na kuleta mashaka juu ya urejeshwaji wa mikopo hiyo, pia nilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa zilitoa Sh. milioni 895.94 kwa vikundi 48 ambavyo havikuwapo," alisema CAG Kichere.

Katika wasilisho la CAG, Rais Samia Suluhu Hassan, fedha za mikopo inayotolewa na halmashauri zipatazo 180 nchini, zimegeuka kuwa kichaka, kwa kuwa ndiko chanzo cha upotevu wa fedha za serikali, akipendekeza mabadiliko yafanyike na sasa itolewe benki.

Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorejewa 2019), kwa kuongeza kifungu cha 37A mahususi kwa ajili ya kuwezesha mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; Kifungu cha 37A (1) cha sheria hiyo kinazitaka halmashauri zote kutenga asilimia 10 ya mapato yao ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyosajiliwa.

Vilevile, Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, 2019 (Tangazo la Serikali Na. 286 la 5/04/2019) zinataka mamlaka zote za serikali za mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Katibu wa SHIVYAWATA anafafanua kuwa utaratibu uliokuwa unatumika siku zote ulifuata kanuni iliyotolewa na TAMISEMI (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa). "Hatujajua masharti yatatumika yapi, ya kibenki au Tamisemi."

"Na kama tutatumia masharti ya kibenki kwakuwa lengo ni mikopo irejeshwe, shaka litabakia kuwa uwezo wa WWU (Watu Wenye Ulemavu) kutimiza masharti hayo.

Wakati mikopo ikitolewa kwenye halmashauri maana yake huduma hiyo ilishuka hadi ngazi ya kata, jirani na makazi ya wakopaji.

Hata hivyo, kukosekana miundombinu rafiki kwa baadhi ya watu wa kundi hilo, kunahitajika marekebisho na ukarabati wa majengo ili WWU waweze kuyafikia kwa urahisi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hii hapa maana ya umma kutakiwa kuzingatia kanuni stahiki za afya

Na Christina Mwakangale

**KATI** ya masuala ambayo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, mara tu baada ya Uhuru, alizama kuyapa msisitizo kwa vitendo, ni kuwapo mikakati suala la usafi katika jamii.

Uhamasishaji ulifika hadi kwenye rekodi za muziki, nyimbo zilieleza umuhimu wa usafi, mfano na ipo nyimbo iliyokuwapo miaka hiyo naikumbuka, 'Mtu ni Afyaa! mwananchi elewaaa...' ulipigwa na Morogoro Jazz.

Ujumbe uliomo na mpangilio wa mashairi, lazima ukisikia utaguswa na kuanza kubadilika taratibu na kuweka maeneo yako kuwa safi.

Wiki iliyopita, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, alihimiza kila mmoja atunze mazingra na kuweka maeneo safi, pamoja na upandaji miti kwa ajili ya kivuli na matunda.

Alisema, usafi wa mazingira ikiwamo wa majumbani, kutotupwa taka ovyo, kunakoendana na upandaji bustani za maua, utaongeza utunzaji mazingira. Kwa nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania, usafi ni kati ya sababu za umaskini, maradhi hususan na lisipotiliwa mkazo kwa wananchi na viongozi wa kila ngazi hasa kimkoa hadi kata, ni hatari kiafya.

Utaratibu wa usafi kila wiki ya mwisho ya mwezi, Jumamosi kuwa maalumu kwa ajili ya shughuli hiyo nchi nzima, inaongeza uwajibikaji wa viongozi kwenye maeneo yao.

Mkoa wa Dar es Salaam, utaratibu huo ulianza tangu sherehe za Uhuru mwaka 2015, ingawa sasa utekelezaji wake ni duni. Wanachokifanya wafanyabiashara na wajasiriamali wanafunga maduka yao hadi ipite saa na kufungua baada ya muda huo, huku wakiacha kufanya usafi.

Hadi sasa, utaratibu umezorota na kufanya maeneo kadhaa kuwa machafu. Utashuhudia hilo zaidi katika maeneo walikokuwa wamachinga na wafanyabiashara wakaondolewa kwa agizo la nchi nzima.

Wakuu wa mikoa walilisimamia ipasavyo, ingawa sasa upo utaratibu biashara kufanyika usiku, Je, usimamizi wa usafi maeneo haya nani anawajibika.?

Kunapokucha asubuhi baada ya biashara usiku kucha, maeneo haya yanakuwa dampo! Uchafu unazagaa. Kwanini utaratibu usiwekwe kusimamia hili? Chupa za vinywaji zenye rangi ya bluu, nyeusi, ndio usiseme zimejaa mitaroni, barabarani na hazikotwi. Waokota makopo wakidai hazifai kurejelezwa.

Mwisho wa siku wafanyabiashara hawa wanaojitafutia riziki, wataonekana hawaendani na taratibu zinazowekwa, lakini nani anawakumbusha, anawasimamia, watu wako huru!

Waelekezwe biashara ndio zifanyike usiku, lakini viongozi wa mitaa, maofisa afya, biashara, wakuu wa Wilaya na mikoa, kulibaini hili, tembeleeni mlikowaondoa wamachinga mitaani.

Uamuzi wa usafi ulioanzishwa, yaani kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi, ilikuwa mwanzo kwa viongozi wa mikoa, wilaya, halmashauri kutekeleza hatua hii kwenye maeneo hayo, na kila kaya, eneo la biashara kuanzia asubuhi hadi saa nne asubuhi kuutumia muda huu kufanya usafi na kusitisha shughuli zao, usafi kwanza.

Hali si nzuri kwa maeneo mengi ya mitaani, barabara zimejaa vumbi, mchanga, taka kwenye mitaro, nafuu ipo katika barabara kuu tu, ndiko kunakofagiliwa kila baada ya siku kadhaa.

Uzoaji taka maeneo kadhaa, umesuasua, mitaa kadhaa ukipita hali ni hiyo, hata sokoni na kuliko na mikusanyiko mingi ya watu, vituo vya daladala.

Baadhi ya maeneo ikiwamo Tegeta, Kunduchi, Bunju, Buguruni, Mombasa, Temeke, Mbagala, Gongo la Mboto kwenye makazi ya watu hali hii ipo.

Wakazi walio wengi kutegemeana na eneo wanaloishi, hulipia ada ya ubebaji taka katika kila kaya kwa kiasi cha shilingi 3,000 ama 5,000 hadi 10,000 kwa mwezi, baadhi ya maeneo taka hazibebwi kwa wakati muafaka.

Nakumbuka watendaji, wakurugenzi wa halmashauri katika mikoa na wilaya nchini, waliagizwa kuhakikisha usafi na uondoshaji wa taka katika maeneo yao unafanyika kabla ya kuchukuliwa hatua.

Walitakiwa kuvunja mikataba kati yao na baadhi ya kampuni za kuzoa taka, hazitekelezi majukumu waliyopewa vilivyo, hata kusababisha ongezeko kubwa la taka mijini. Ifahamike, kati ya asilimia 80 hadi 90 ya taka zinazozalishwa mijini, hazikusanywi na mamlaka husika.

# Wanafunzi 29 UDSM wapata tuzo mashindano stadi za kufundisha

**Na Mwandishi Maalum**

WANAFUNZI 29 kati ya 105 wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wamepewa tuzo ya ushindi katika mashindano ya Kwanza ya Stadi za Kufundisha.

Mashindano hayo yaliyoandaliwa kwa pamoja na Chuo cha Elimu (SoED), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kituo cha Pamoja cha Utafiti wa Elimu cha China na Afrika (SA-JoCER), yanalenga kuwawezesha walimu wanafunzi kuonesha umahiri, uwezo na ubunifu wao.

Kwa mujibu wa Tovuti ya Serikali ya China, Mkuu wa Shule ya Elimu (SoED) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Eugenia Kafanabo, alisema mashindano hayo yanalenga walimu wanafunzi ambao wako katika mwaka wao wa pili na wa tatu wa masomo.

"Mashindano ya stadi za kufundisha yalilenga kuongeza uelewa wa umuhimu wa vitendo na kuboresha miundo ya ufundishaji."

Kafanabo alisema, mashindano hayo yamehusisha masomo 10 tofauti ambayo yalichaguliwa kutoka katika mihtasari ya shule za sekondari, yakiwamo masomo ya Biolojia, Kemia, Fizikia, Hisabati, Uraia, Historia, Jiografia, Kiswahili, Kiingereza na masomo ya lugha ya Kichina.

"Mashindano haya yanaweza kuwa kiingilio cha kuwaleta pamoja wadau wote husika kama muungano wa kuchangia ubora wa elimu ya walimu," alisema Eileen Xu, Mratibu wa SA-JoCER, iliyoanzishwa kwa pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ualimu cha Zhejiang cha China.

Mkurugenzi wa Elimu ya Msingi katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya Tanzania, Venance Manori, amekipongeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ualimu cha Zhejiang kwa kuandaa mashindano hayo, ambayo alisema yataboresha ujuzi wa kufundisha walimu wa Tanzania.

# Wasafirishaji mboga, matunda waomba kuboreshewa miundombinu

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

WASAFIRISHAJI wa mboga na matunda mkoani Njombe, wameiomba serikali kuboresha miundombinu ya usafirishaji wa bidhaa hizo ili zifike sokoni kwa wakati na ubora.

Ombi hilo limetolewa katika mkutano wa uhamasishaji wa usafirishaji wa mazao ya mboga na matunda kwa njia ya meli na viwanja vya ndege vya ndani ya nchi ulioandaliwa na Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC), Taasisi ya Kikanda ya Uchukuzi (ISCOS) pamoja na Baraza la Wasafirishaji Tanzania (TSC).

Akizungumza na Nipashe mmoja wa wasafishaji, Zekomo Masanje, aliomba kuwapo kwa majokofu ya kuhifadhi baridi, bandari kavu na kuondolewa vikwazo vya usafiri barabarani ili magari yafike haraka.

"Changamoto kubwa ni kontena za friji ambazo kwa sasa zinapatikana Nairobi, kwa hiyo unakuta kuna gharama kubwa na pia hizo kontena tunatumia bandari ya Mombasa ambapo unakuta kuna gharama kubwa katika usafirishaji unakodi kutoka Nairobi ije Njombe, itoke Njombe iende Mombasa. Tunashauri kama kuna uwezekano serikali yetu iweke utaratibu mzuri kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam," alisema Masanje.

Katibu Mtendaji wa Baraza la usafirishaji shehena Tanzania, Sallu Jonhsons, alisema changamoto kubwa inayowakabili wasafirishaji shehena, ni ucheleweshaji wa usafiri wa mizigo kutoka shambani kuelekea bandarini.

"Kama Bandari ya Dar es Salaam, Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam, Uwanja wa KIA, tunapata matatizo kwa sababu ya changamoto, kuna mizani, watu wa usalama... nafikiri ikiwezekana gari inavyotoka Njombe ikipimwa uzito na kukidhi taratibu zote za barabara watu wa TANROAD wakatoa cirtificate hakuna sababu gari kuendelea kusimamishwa hadi kufika Dar es Salaam," alisema Johnson.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, aliomba kuwekewa majokofu katika bandari kavu inayotarajiwa kuanzishwa Halmashauri ya Mji Makambako.

"Tuna mpango wa kuanzisha bandari kavu Makambako ili kuhakikisha uchumi huu ambao mnauona unakuwa wa Njombe, tunakuwa tuna sehemu ambayo watu wanatoka nchi za jirani ambazo zimepakana na Nyanda za Juu Kusini, wafike waweke bidhaa zao zote center kubwa iwe Makambako," alisema Kasongwa.

Mkurugenzi wa Udhibiti wa Huduma za Usafiri kwa njia ya maji TASAC Deogratius Mukasa, alisema lengo la mkutano huo ni kupokea changamoto ili zikafanyiwe kazi kuhakikisha huduma za usafirishaji zinawafikia.

"Lengo ni kuwawezesha wasafirishaji wa ukanda huu wa Nyanda za Juu Kusini wanaotumia huduma za bandari kusafirisha bidhaa nje ya nchi kupata uelewa juu ya namna bora ya kutekeleza majukumu yao usafirishaji kwa namna wanavyoweza kulinda maslahi yao katika kutumia huduma za usafirishaji," alisema Mukasa.

Mwakilishi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA), Robert Soko alisema, maboresho makubwa yamefanyika ili kuvutia wasafirishaji wa mali mbichi nchini kutumia usafiri wa meli.

Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Uchukuzi (ISCOS), Aderick Kagenzi, alisema teknolojia inatumika ili kukabiliana na changamoto za usafirishaji.

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

## TANGAZO LA NOTISI YA KUONDOKA KWA WAGUSWA WA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP)

**Tarehe ya Tangazo : 19 April 2023.**

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika ya Mashariki ni njia ya bomba itakayosafirisha mafuta ghafi yatakayozalishwa kutoka viunga vya mafuta vya Ziwa Albert nchini Uganda mpaka bandari ya Tanga, nchini Tanzania ambapo mafuta hayo baadae yatasafirishwa kwenda kwenye masoko ya kimataifa. Bomba litafukiwa chini na litatandazwa urefu wa kilometa 1,443 kuanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Rasi ya Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania, ambapo asilimia 80 ya urefu wa bomba ipo nchini Tanzania na asilimia 20 ipo upande wa Uganda.

Utwaaji wa Ardhi kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika ya Mashariki unasimamiwa kwa Pamoja na Kampuni ya Mradi wa EACOP Pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) huku pia wakishirikiana na mamlaka nyingine za Serikali katika Mikoa 8 (Kagera, Geita,Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga) ambayo bomba litapita.

Baada ya zoezi la uthamini wa Ardhi na Mali nyingine zisizohamishika, kuonyeshwa stahiki pamoja na utiaji saini mikataba ya fidia kwa waguswa wa mradi, Waguswa wote waliosaini mikataba yao ya fidia, wamepokea malipo yao ya fidia isipokua kaya chache zinazoguswa Makazi ambazo zilichagua fidia ya nyumba mbadala. Ujenzi wa Nyumba hizi unaendelea na zitakabidhiwa kwao mara tu baada ya ujenzi kukamilika.

TPDC, kama Mtwaaji wa Ardhi kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, imetoa Notisi ya Kuondoka ya Miezi Mitatu (3) kuanzia Tarehe 01 Mei 2023 mpaka Tarehe 31 Julai 2023. Baada ya Tarehe 31 Julai 2023, waguswa wote wanatakiwa wawe wameondoka na kuacha kutumia ardhi iliyoguswa na mradi.

Waguswa wanaruhusiwa kutumia ardhi zao mpaka tarehe 31 Julai 2023 lakini hawaruhusiwi kupanda mazao ya kudumu au miti, kujenga majengo mapya au kuboresha majengo yaliyopo na kufanya shughuli za maziko katika kipindi cha Notisi ya Kuondoka kwani hakuna fidia ya nyongeza itakayotolewa kwa mazao au matumizi mengine ya ardhi katika kipindi hiki.

Kaya zilizoguswa Makazi ambazo zilichagua **Fidia ya Fedha Taslimu** zinapaswa ziwe zimeondoka kwenye nyumba au ardhi zilizoguswa na mradi itapofika tarehe 31/07/2023. Mradi utatoa usaidizi wa kuhamishwa kwenda maeneo ya karibu na eneo lililoguswa na Mradi.

Kaya zilizoguswa Makazi ambazo zilichagua **Fidia ya Nyumba Mbadala** zitapaswa kuondoka kutoka kwenye nyumba au ardhi zilizoguswa na mradi mara tu **baada ya ujenzi wa nyumba zao kukamilika na wao kuhamishiwa kwenye makazi yao mapya**. Taarifa za ziada zitatolewa kwa kaya hizi na Mradi utawapatia usaidizi wa kuhamishwa kwenda Nyumba zao Mbadala.

Mradi unawakumbusha Waguswa wote wa ardhi na makazi katika maeneo ya Miundombinu ya Juu na Barabara zake ambao walipokea Notisi zao za kuondoka Tarehe 06 Februari 2023 kwamba wanatakiwa kuondoka kwenye ardhi zao itapofika Tarehe 06 Mei 2023.

Waguswa wawasiliane na Mradi kwa njia zifuatazo:

- Kupiga simu namba ya bure **0800780068**
- Kuandika barua pepe **info.tz@eacop.com**
- Wasiliana na Mwenyekiti au Mtendaji wa Kijiji/Mtaa

217382001

# ‘Imani potofu chanzo uwindaji haramu Babati’

**Na Jenifer Gilla, aliyekuwa**
BABATI

WAKAZI wa Kijiji cha Ngoley, Halmashauri ya Wilaya ya Babati, wamesema kuenea kwa taarifa potofu kuwa nyama ya porini inatibu baadhi ya magonjwa ya binadamu inachangia kuwapo kwa uwindaji haramu katika mapitio ya wanyamapori (shoroba) ya Kwakuchinja.

Mmoja wa wanakijiji hao, Luciana Martin, aliiambia Nipashe kuwa kumekuwa na taarifa kuwa nyama ya punda inatibu ugonjwa wa kifua huku makongoro yake yakitibu matatizo ya miguu hali inayosababisha watu wengi wenye matatizo hayo kuagiza nyama hiyo.

Alisema cha ajabu ni kuwa licha ya wagonjwa wenye matatizo hayo kutumia nyama hiyo bado wanaendelea kusumbuliwa na magonjwa hayo hali inayoonyesha kuwa taarifa hizo sio za kweli bali zimetungwa na wafanyabiashara haramu kama njia ya kujipatia fedha.

“Miaka ya nyuma na mimi niliingia kwenye huo mtego kwa kuwa nilikuwa nasumbuliwa na kifua, nikawa natumia hiyo nyama, lakini sikupona ndio kwanza hali ilikuwa mbaya kwa sababu niliacha kutumia dawa za hospitali, tangu nilipoacha kula hiyo nyama na kutumia dawa za hospitali sasa nimepona kabisa,” alisema.

Gideon Daniel alisema, baadhi ya wanyama wanaodaiwa kutibu maradhi ni nyumbu na digidigi ambaye alishawishika kuagiza nyama ya nyumbu baada ya kuambiwa kuwa inatibu maradhi ya figo, lakini baada ya kuitumia kwa siku kadhaa hakuona mafanikio na kuamua kuachana nayo.

Gideon aliwaomba askari wa wanyamapori kwa kushirikiana na polisi jamii kuendesha doria ya siri ili kuwakamata watu wanaoeneza uzushi huo kwa manufaa yao binafsi kwa kuwa licha ya kuhamasisha uvuvi haramu, pia jamii inapata madhara makubwa kutokana na nyama hizo ikiwamo kuinyima nchi kipato na utalii.

Magret Mandao alisema, ulaji wa nyamapori waliowindwa bila kibali una madhara ya kiafya kwa kuwa wakati mwingine unaletewa nyama yenye madhara kwa binadamu bila kufahamu.

“Miaka ya nyuma niliuguza mtoto, alikula nyamapori ambayo mpaka leo sijui ni mnyama gani, akavimba mdomo na ukawa mwekundu, tulihangaika sana hospitali, ilichukua muda mrefu kupata tiba, kwa hiyo tusisikilize maneno ya hawa jamaa, hii nyama sio salama kwa kuwa haijapitia njia za salama za uwindaji,” alionya.

Chifu wa kitongoji wa Eluway, Leteiva Loburu, alisema watu hao huwashawishi wanawake kuwa nyama hizo zinatibu magonjwa kwa kuwa wamewaona ni kundi linaloamini taarifa kwa urahisi bila kuzifanyia uchunguzi.

Aidha, alisema anawashukuru wadau wa uhifadhi wanyamapori ikiwamo taasisi ya kijamii ikiwamo Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Burunge (JUHIBU), Community Support Initiative Tanzania (COSITA) kwa kushirikiana na Askari wa Usalama Barabarani (TRAFFIC) kwa kuwapa elimu kuhusu madhara ya kuwinda wanyamapori kwa jamii ambayo imesaidia kupunguza matukio hayo.

Katibu wa JUHIBU, Benson Mwaise, anasema wanashirikiana wadau wengine wa uhifadhi ikiwamo TAWA na USAID, kutoa elimu kwa jamii kuhusu uzushi kama huo wenye lengo la kuchochea uwindaji haramu na wanashukuru kuwa mwitikio ni mzuri.

“Kupitia elimu jamii imeelewa imeona umuhimu wa kuhifadhi maliasili hii muhimu kwa utalii nchini, sasa hivi na wenyewe wanashiriki kuitunza, hata wakiona swala amepotea au ameumia watatoa taarifa au kumleta hapa ofisini, kwa kweli tunashukuru wadau ikiwamo USAID wanaotuunga mkono mafanikio ni makubwa,” anasema.



Mwanaharakati Dk. Azaveli Lwaitama (kulia) na wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakitoka katika Mahakama Kuu kanda ya Dar es Salaam jana, baada ya kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama wa wabunge 19 akiwemo Halima Mdee wa chama hicho, kuahirishwa. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Kesi ya kina Mdee yapigwa kalenda

**Na Grace Gurisha**

KESI ya kupinga kuvuliwa uanachama iliyofunguliwa na wabunge 19 wa Viti Maalum kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), imeahirishwa kusikilizwa hadi Mei 17, kwa kuwa jaji anayeisikiliza kesi hiyo hatokuwapo.

Kesi hiyo ilitarajiwa kusikilizwa jana mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wa Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam kwa hatua ya mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa Chama hicho, Lucy Mollel kulizwa maswali ya dodoso na mawakili wa wabunge hao.

Msajili wa Mahakama hiyo, Veronica Mteta aliahirisha kesi hiyo hadi Mei 17, mwaka huu kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa.

Machi 6, wakili wa wajibu maombi, Ipilinga Panya, aliomba mahakama itoe hati za wito za wajumbe saba wa bodi hiyo kujibu maswali ya dodoso kuhusu viapo vyao kinzani katika maombi hayo.

Aliwataja wajumbe hao kuwa ni Silvester Masinde, Profesa Azaveri Lwaitama, Lucy Mollel, Mary Joakim, Francis Mushi, Maulida Komu, Ahmed Hamis, ambao wanataka kuwahoji kutokana ana vitu ambavyo wamevieleza katika kiapo kinzani cha Chadema.

Mdee na wenzake walifungua shauri hilo namba 36/2022 Julai 22, 2022 wakiomba Mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama na pia iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza.

Pia, wanaomba amri ya zuio dhidi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutokuchukua hatua yoyote hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

# Kanisa laomba Watanzania kumuunga mkono Rais Samia

**Na Joseph Mwendapole**

MWENYEKITI wa Wazazi CCM Mkoa wa Morogoro, Dk Rose Rwakatare amewaomba watanzania kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwa kukemea mmomonyoko wa maadili ili kuwa na kizazi chenye maadili mema.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki kwenye kongamano la uamsho wa ndoa lililofanyika kwenye Kanisa la Mlima wa Moto Mikocheni jijini Dar es Salaam.

Alisema kongamano la uamsho wa ndoa lilianzishwa mwaka 2,000 kupitia maono ya mwanzilishi wa Kanisa la Mlima wa Moto, Hayati Askofu Getrude Rwakatare.

Aidha, Dk. Rose alisema kuna wimbi jipya linaitesa dunia la ndoa za jinsia moja na yeye kama Mwenyekiti wa Wazazi Mkoa wa Morogoro amekuwa mstari wa mbele kupinga vitendo hivyo kwani havitaleta mustakabali mwema kwa Taifa la Tanzania.

“Tumuunge mkono Rais wetu Samia Suluhu Hassan, hili ni pepo ambalo tunapaswa kulikemea kwa nguvu zetu zote, tunapaswa kusali kwa bidii ili liondoke, kama majanga mengine ambayo tulipiga magoti yakaondoka hili nalo kwanini tusiombe likaondoka, wazazi tusimame kwa umoja wetu kupinga jambo hili,” alisema.

Alisema kutokana na huduma kubwa ambayo Mungu alimkirimia kuhudumia waumini wa kanisa na katika huduma zote Mungu alizomwitia, hayati Getrude Rwakatare, alitilia mkazo watu kupendana na kuheshimiana na ndipo akaanzisha uamsho wa ndoa.

“Askofu Rwakatare alipenda wanandoa waishi kwa upendo ili ndoa ziweze kudumu na kuwa bora na zilizojaa amani na utulivu kwani hapo ndipo afya ya akili inapokuwapo na kuwa na familia bora,” alisema.

Alisema kwa kushirikiana na wazee wa kanisa hilo na askofu wa kanisa hilo, Askofu Rose Mgeta wamefanikisha kuendeleza tukio la uamsho wa ndoa kwa miaka yote na wamekusanyika kufanya uamsho wa ndoa ili ziweze kupona na kuwapa amani ya moyo wana ndoa. Naye Askofu Mkuu wa Kanisa la Mlima wa Moto, Mikocheni jijini Dar es Salaam, Bishop Rose Mgeta alisema kanisa hilo litaendelea kutekeleza maono ya Mwanzilishi wa Kanisa hilo, Hayati Askofu Dk Getrude Rwakatare kutimiza maono yake kama kuendeleza makongamano ya uamsho wa ndoa kila mwaka.

Hayati Dk. Getrude Rwakatare alianzisha kongamano la uamsho wa ndoa mwaka 2000 kwa lengo la kuhakikisha anaokoa ndoa nyingi baada ya kuona ndoa nyingi zikiingia kwenye mogogoro na kusababisha watoto wengi kuachwa mitaani.

Askofu Mgeta alisema kupitia tukio la uamsho wa ndoa, ndoa nyingi zimepona kutokana na shuhuda mbalimbali zilizokuwa zikitolewa na watu waliokuwa wanahudhuria makongamano hayo.

Alisema hata watoto wa hayati Getrude Rwakatare wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha ndoto za mwanzilishi wa Kanisa hilo zinatimizwa.

Askofu Daniel Mgogo alisema amekuwa akitoa mafundisho mbalimbali ya ndoa kwenye mitandao ya kijamii lakini kwa muda wa miezi sita hakuandika chochote kwani alikua nchini Marekani.



# CCM yakataa mradi kituo cha afya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUMERU

WAJUMBE wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, wamekataa kupokea mradi wa Kituo cha Afya cha Mateves, kutokana na kujengwa chini ya kiwango huku nyufa zikianzia kwenye msingi.

Akizungumza wakati wa ziara ya kamati hiyo, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya hiyo, Noel Severe, alisema wajumbe wamekataa kupokea mradi huo kutokana na kushuhudia madudu mbalimbali.

Kadhalika wataalamu wa ujenzi huo, wameshindwa kueleza gharama za mradi unaojengwa kwa mapato ya ndani ya Halmashauri ya Arusha.

"Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya tumekataa kupokea mradi wa kituo hiki cha afya cha Mateves kwa sababu kimejengwa chini ya kiwango. Kina nyufa kila mahali wakati Rais Samia Suluhu Hassan anahangaika kutafuta fedha kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora huku wengine wakichezea fedha hizi," alisema.

Alisema wakiwa wasaidizi wa Rais, hawatakubali kuona wataalam wa halmashauri wakihujumu kazi anayoifanya ya kutafuta fedha za miradi ya maendeleo.

"CCM Wilaya ya Arumeru hatutakubali watendaji wa Halmashauri ya Arusha watuchonganishe na wananchi ambao mwaka 2020 tuliahidi mambo kadha wa kadha na wakatuamini wakatupa ridhaa ya kushika dola. Nimwombe mkurugenzi kuanzia sasa ahakikishe thamani ya miradi inaakisi fedha iliyotumika," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wa Mateves, Diwani wa Kata hiyo, Freddy Lukumay, alisema mradi huo umejengwa chini ya kiwango kwa sababu hakuna ushirikishwaji wa wananchi wala viongozi wa eneo hilo, hali inayosababisha washindwe kuhoji.

"Changamoto kubwa wananchi hawashirikishwi na viongozi juu ya miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao ili kufuatilia kwa karibu hali ambayo inayosababisha miradi kutokidhi vigezo vinavyohitajika," alisema.

Kaimu Mhandisi wa Halmashauri hiyo, Sharif Said, alisema ujenzi wa jengo hilo uko kwenye hatua za umaliziaji na zinahitajika Sh. milioni 98 kwa ajili ya kukamilisha kazi iliyosalia.

Baada ya majibu hayo, alipoulizwa iwapo fedha hizo zitatosha na zitafanya kazi gani, alishindwa kutoa majibu huku akiwa hajui gharama halisi ya mradi huo.

Kutokana na majibu hayo, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Noelia Kaganda, alisema siku tatu zilizopita Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ilifika kwenye jengo hilo kuangalia tatizo hilo. Alisema Mhandisi Said alishindwa kueleza gharama za mradi na kuagizwa kabla ya kamati ya siasa ya wilaya kufika kwenye mradi huo, awe na taarifa kamili lakini hakufanya hivyo.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Kamati ya Usalama ya Wilaya tulikuwa hapa na mhandisi huyu alishindwa kutueleza gharama za mradi, nikamwagiza tukifika hapa na kamati ya siasa tumkute akiwa na gharama halisi za mradi lakini hajafanya hivyo," alisema.

"Sasa ninakuagiza tena aondoka kwenye ziara hii mara moja, uende ukandae taarifa kamili ya huu mradi ikiwa ni pamoja na gharama halisi za mradi, nizikute ofisini kwangu asubuhi," alisisitiza.

## Miti 170 kupandwa kuhifadhi mazingira

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

ZAIDI ya miti 170,000 inatarajiwa kupandwa na serikali Simanjiro mkoani Manyara, kwa lengo la kuhifadhi mazingira na kubabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Kati ya miti hiyo, 20,000 itatekelezwa kwa kutumia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kupitia mradi wa kusaidia kaya maskini. Wilaya ya Simanjiro misitu yake mingi ni miti ya asili iliyotawaliwa na miti aina ya migunda na mipone. Kwa mwaka jana ilipandwa miti 67,854 kwenye maeneo tofauti.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk.Suleiman Serera, alisema jana aliongoza upandaji mti kwenye kijiji cha Naepo katika Kata ya Naisinyai kupitia kaulimbiu ya "Mazingira Yangu, Nchi Yangu, Naipenda Daima".

Dk. Serera alisema miti hiyo, itapandwa kwenye maeneo tofauti yakiwamo ya taasisi za serikali kwenye ofisi za vijiji, ofisi za kata, shule, zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Ili kufanikisha azma hiyo, aliagiza wananchi kupanda miti kwenye makazi yao ili kwenda sambamba na kaulimbiu hiyo ya wilaya.

"Kila kaya inapaswa kupanda miti 10 kwenye makazi ikiaemo miti ya vivuli na matunda kwa ajili ya kujipatia lishe, hivyo jamii itekeleze hayo na miche inapatikana kila mahali," alisema Dk. Serera.

Mratibu wa TASAF wa Wilaya ya Simanjiro, Mathias Nyangusi, alisema kupitia mradi wa kuhifadhi mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, pia kaya masikini zitanufaika.

"Mradi huu umekuwa msaada kwa kaya zenye uhitaji mkubwa kujipatia mahitaji ya familia,kuanzisha shughuli za ujasiriamali na uboreshaji makazi ya walengwa," alisema Nyangusi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Naepo, Anna Yusuf, alisema wamejipanga kuhakikisha miti inastawi na kukua kwa kushirikiana na walengwa wa mpango wa huo.




Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (katikati), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kupokea majokofu sita ya mnyororo wa baridi yenye thamani ya Sh. milioni 600 kutoka kwa Vodacom Tanzania Foundation na Vodacom Group, Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya kuhifadhia chanjo ili kuimarisha mpango wa Taifa wa chanjo nchini. Wengine ni Mwenyekiti wa Vodacom Tanzania Foundation, Harriett Lwakatare (kushoto) na Mkurugenzi wa Fedha wa Vodacom Tanzania, Hilda Bujiku. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

## Miundombinu shule 190 serikali chakavu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro, imesema shule za msingi za serikali 190 kati ya 229 zinakabiliwa na uchakavu wa miundombinu katika hali tofauti, hivyo zinahitajika kukarabatiwa na zingine kujengwa upya.

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Gaudence Assey, alisema hayo jana wakati akizungumza katika hafla ya kukabidhi matundu tisa ya vyoo, vifaa vya ukarabati wa madarasa na vyakula vilivyotolewa na shirika lisilo la kiserikali la Rawuya Foundation katika shule ya msingi ya Mkolowony iliyoko Kata ya Mamba Kusini.

Alisema uchakavu huo umesababishwa na shule hizo kujengwa miaka mingi iliyopita kuanzia mwaka wa 1940.

"Shule hizi zmejengwa miaka ya 1940 na nyingi hazijawahi kufanyiwa ukarabati mkubwa, zingine zina nyufa, paa zinavuja, vyoo vimetitia lakini serikali imeshaanza mkakati wa kuzifanyia ukarabati na kuzijenga upya," alisema.

Alisema mwaka wa fedha wa 2022/23 ilituma fedha kwa ajili ya kuanza kufanya ukarabati lakini bado kuna nafasi kwa wadau kusaidia ukarabati huo kwa kufuata sheria na taratibu za nchi.

Pia alisema wanapendekeza wanafunzi waliosoma kweye shule hizo wajitolee kusaidia kufanya ukarabati na shughuli zingine za maendeleo.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Augustina Moshy, alisema shule hiyo inakabiliwa na matatizo mengi yakiwamo ukosefu wa maji ya uhakika, uchakavu wa miundombinu na uhaba wa walimu.


"Katika shule yetu kuna uchakavu mkubwa wa miundombinu, nyufa katika kuta na paa kuvuja hasa nyakati za mvua. Pia tulikuwa tunakabiliwa na tatizo la matundu ya vyoo lakini kwa sasa tumepata wafadhili wametujengea na ingawa bado tuna ukosefu wa choo cha walimu," alisema.

Emmanuel Kimei, ambaye ni Mwenyekiti Rawuya Foundation, alisema lengo la uanzishaji wa taasisis hiyo ni kukabiliana na matatizo katika jamii ili kuona fursa, kujinyanyua kiuchumi na kufanya kilimo chenye tija kitakachonyanyua uchumi wa wananchi wa chini.

"Tulivutiwa sana kuanza kutoa msaada katika shule hii kutokana na mazingira yake. Ukarabati wa choo hiki ni zaidi ya Sh. milioni 25 na tumeleta vyakula yakiwamo mahindi na maharage kwa kuwa kutokana na utafiti wetu, watu wa hapa wanashindwa kuwahudumia watoto chakula," alisema.

Mmoja wa wanafunzi waliopokea msaada huo, Gean Masawe, aliomba serikali kuangalia namna ya kufanya ukarabati katika shule mbalimbali nchini ili kuwajengea wanafunzi mazingira rafiki kwa ajili ya kujifunzia.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Diwani wa Mamba Kusini, Elirehema Tesha, aliwataka wazazi kuacha kubweteka katika uchangiaji wa chakula kwa watoto na kusisitiza kuwa suala hilo ni jukumu la mzazi.





# Polisi waombwa kuwahifadhi watoa taarifa za wizi SGR

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BAADHI ya wananchi wa Kata ya Chibe mkoani Shinyanga katika eneo linalopitiwa na reli ya kisasa (SGR) kutoka Isaka hadi Mwanza wameliomba Jeshi la Polisi kutunza siri za watoa taarifa juu ya wizi wa vifaa vya ujenzi wa reli hiyo.

Imedaiwa kuwa wizi huo umekithiri kutokana na taarifa zinazotolewa mara kadhaa kuvuja hali inayohatarisha maisha yao.

Wananchi hao ambao hawakutaka majina yao kutajwa, walisema hofu yao juu ya utoaji wa taarifa za wahusika wa wizi wa vifaa vya mradi huo ni pale baadhi ya askari polisi wasio waadilifu wanapozivujisha na wahusika kuanza kuwalipizia visasi hali inayowafanya wasusie kutoa taarifa.

Akizungumza na wananchi hao juzi wakati wa kampeni ya Kataa Uhalifu, iliyoandaliwa na Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, alikemea vitendo vya baadhi ya wananchi kuhujumu mradi huo kwa kuiba vifaa vya ujenzi pamoja na mafuta hali ambayo imekuwa ikikwamisha mradi huo.

Alisema wananchi wanatakiwa kuwafichua wahalifu ambao wamekuwa wakiuhujumu mredi kwa kuiba vifaa mbalimbali vya ujenzi na mafuta ili washughulikiwe kutokana na mradi huo kuwa kichocheo kikubwa cha uchumi ndani na nje ya nchi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, aliwaomba wananchi kushirikiana na jeshi hilo katika kuwapatia taarifa za uhalifu kwa watu ambao wamekuwa wakijihusisha kuhujumu mradi huo ili wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Aliwahakikishia wananchi hao kuhusu utunzaji wa siri zao na kuwaahidi kuwa hakuna siri yoyote itakayotolewa endapo watawabaini wahusika huku akiendelea kuwashukuru wananchi ambao wamekuwa wakiendelea kutoa taarifa za uhalifu, hasa kwa wale ambao wamekuwa wakihujumu mradi huo.




Mkurugenzi wa Ujenzi na Uendeshaji wa Vivuko wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), Mhandisi Sylvester Simfukwe (kushoto) na Mkurugenzi wa Huduma Saidizi, Josephine Matiro wakiwaongoza wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya wakala huo, wakati wakishuka kutoka kwenye kivuko cha MV Misungwi kinachokarabatiwa baada ya kukagua katika yadi ya Songoro, jijini Mwanza juzi. **PICHA: WUU**

# Tarime wazidi kudhibiti ukatili kijinsia

**Na Timothy Itembe,** TARIME

SERIKALI imeendelea kuonyesha nia ya kudhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia ukiwamo ukeketaji ambao ulikuwa umekithiri katika maeneo mbalimbali Wilaya ya Tarime mkoani Mara.

Vitendo hivyo vya ukeketaji vimekuwa vikitekelezwa na watu wenye mila potofu wakidai kunusuru ndoa zao.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Anthony Nyange, alisema hayo juzi wakati akizungumza na gazeti hili na kuweka bayana kwamba kuwa tayari serikali imeweka mipango mbalimbali ukiwamo ule wa kuwasaidia waathirika wa vitendo hivyo kwa kuwapatia mikopo. Alisema juhudi ambazo zimekuwa zikifanywa na wadau mbalimbali kwa kushirikiana na serikali ikiwamo kuwakamata na kuwafungulia mashtaka wahusika wa vitendo hivyo zimesaidia kuvipunguza na kufanya hali kuwa salama kwa sasa.

"Tunatoa mikopo kwa wanawake na vijana waliathirika na ukatili huku watoto wadogo tukihakikisha wote wanakwenda shuleni na kupata elimu. Kadhalika, idadi ya wanaume waliokuwa wakiwapiga wanawake imepungua kutokana na kukosa kazi hali inayowafanya wanawake kuwa sehemu ya kuhudumia familia zao," alisema.

Alice Mtuga, Ofisa Mawasiliano wa shirika lisilo la kiserikali la Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF lenye makao makuu Dar es Salaam, alisema ushirikiano wanaoupata kutoka serikalini umekuwa chachu katika kupambana na vitendo hivyo.

Pia alisema wamewasaidia wasichana 40 waathirika wa ukeketaji kwa kuwapa mafunzo ya ufundi na ujasiliamali ili kujikimu kimaisha na wengi wao wanafanya shughuli binafsi za kujipatia kipato.

Mmoja wa waathirika, (jina tunalo) mkazi wa Kata ya Mbogi wilayani Tarime, alisema alifanyiwa ukatili huo ikiwa ni sehemu ya kuinusuru ndoa ya mama yake ambaye alitakiwa kuchagua kati ya kufukuzwa au yeye kukeketwa. Aliiomba jamii kuacha mila hizo ambazo zimepitwa na wakati.

# Milioni 493/- kukarabati na kujenga barabara zilizoharibiwa na mvua

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BARABARA yenye urefu wa kilometa moja iliyoharibiwa na mvua hivi karibuni katika Kata ya Nyamilangano, Halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, zimetolewa Sh. milioni 493.6 kwa ajili ya ukarabati wake.

Mbali na ukarabati huo, barabara hizo zinatarajiwa kujengwa kwa kiwango cha lami na kuwekewa taa ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya chakula na biashara kwenda sokoni.

Diwani wa Kata hiyo, Robert Mihayo, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mpango wa kurekebisha barabara zilizoharibiwa na mvua za masika zinazoendelea kunyesha.

Alisema wamepokea Sh. 493, 626, 180 za ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa moja kwa kiwango cha lami utakaotekelezwa na Kampuni ya Bakwema Co. Ltd na kuahidi kusimamaia ujenzi huo na kuhakisha unakamilika kwa muda uliopangwa.

Aidha, Mihayo alisema mpaka sasa wana kilometa tano na mita 400 za barabara zenye kiwango cha lami na kati ya hizo, kilometa nne zimekamilika na kufungiwa taa za barabarani 100 na kilometa moja na mita 400 zinaendelea kujengwa.

Pia alisema uwapo wa taa za barabarani umesaidia wafanyabishara wadogo kufanya biashara zao hadi nyakati za usiku na kujiongezea kipato cha kaya kulinganisha na kipindi cha nyuma na wanazitunza ili zisiharibiwe na kuwakwamisha katika shughuli zao za kibiashara.

"Kati ya kata 20 zilizopo Halmashauri hii kata yangu ya Nyamilangano ndio yenye mtandao mkubwa wa barabara za lami na taa zake kulinganisha na kata nyingine, wachuzi wanafanyabiashara zao usiku na mchana na kujiingizia kipato, sasa tunauwezo wa kusafirisha mazao ya biashara kutoka shambani hadi sokoni bila shida yoyote"Alisema Mihayo.

Mmoja wa wachuuzi Penina Samweli alisema, ujenzi wa barabara hizo zimesaidia pia vijana wao kupata kazi za muda, kujiingizia kipato na kuondokana na kushinda vijiweni wakibishana masuala ya kimchezo ya simba na yanga, nao mama ntilie wakiwauzia chakula wakati ujenzi ukiendelea.

Lucas Mabula alisema hata vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto hasa wa kike vilivyokuwa vinafanywa nyakati za usiku, ikiwamo ubakaji, navyo vimepungua kwa sababu ya taa za barabarani.

Alisema watoto wanapotumwa dukani na wazazi au walezi kwenda kununua mahitaji ya nyumbani, wanaonekana na kurejea salama, hivyo kuomba ujenzi unaoendelea usimamiwe na kukamilika kwa wakati.



Ukurasa 12

**CAG alivyogonga hodi kwa Msajili, vyama vya siasa akikuta 'madudu'**



Ukurasa 13

Mapigano moto Sudan, jirani Kusini, Kenya na Djibouti wajitosa usuluhishi



Ukurasa 14

**Mkumbuke aliyekuwa Katibu Mkuu wa UN, pia Rais Dk. Kurt Waldheim**


siasa

JUMATANO APRILI 19, 2023

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


# Uwekezaji wa Samia katika nguvukazi ya maelfu na ishara anakoelekeza nchi


**Na Mwandishi Wetu**

NI ndani ya kipindi kifupi kumeshuhudiwa sehemu ya hatua kubwa ambayo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amechukua kukimu mahitaji ya umma na mahsusi eneo la ajira.

Mwaka uliopo 2023, una aina ya uamuzi unaobeba tafsiri yenye sura kuu mbili kwa uchumi kitaifa; kuwekezwa katika mahitaji makuu ya huduma za kiserikali, hali kadhalika penye kilio cha taifa na dunia kwa jumla, ajira.

Vilevile inaangukia nadharia ya kiuchumi kwamba katika vyanzo vikuu vya uzalishaji mali vinavyopatikana katika nguzo kuu nne, nguvukazi inaongoza kwa umuhimu; kisha zipo, mtaji, ardhi na ujasiriamali wenyewe unavyofanyika.

Mara zote, nguvukazi ya binadamu ndio inayobaki na nafasi kubwa kutokana na ukweli wake inaratibu uzalishaji na wakati huohuo kufanikisha lengo, kupitia ujuzi na maarifa yake. Kwa hiyo, nchi inapowekeza katika nguvukazi, inabeba maana kubwa.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika mkutano Sikukuu ya Wafanyakazi. **PICHA: MTANDAO**

Pia, nguvukazi hiyo hiyo katika msingi wake kiuchumi inachukua sura mbili katika ufanikisha uzalishaji. Hapo kuna kupatikana vitu halisi kama vile bidhaa zilizopo dukani, au huduma inayokusudiwa, mathalan usafiri na masomo darasani.

Hilo nalo linaporejewa katika uamuzi wa kiserikali uliofanywa na Rais Dk. Samia, akifungua mlilango ya ajira serikali kwa vijana walimu na watumishi wa afya 21,200 ni aina ya neema kwa umma.

Ikirejewa hali halisi iliyoko katika umma, ni takriban kila mwaka kuna waombaji kazi milioni moja wanaomwagwa mtaani kwa mujibu wa Waziri wake wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba.

Uamuzi wa Rais, unabeba sura nyingine kwamba ni dhamira ya kiutawala kuboresha maisha ya wananchi wake katika huduma hizo mbili, afya na elimu.

Huduma ya afya, sasa iko waliko wananchi na inaendeshwa na Mpango wa Afya ya Msingi (MMAM) ulioanza kutumika mwaka 2008, katika zama za uongozi wa nchi awamu ya nne, kupigania kila kijiji au kitongoji kuwa na zahanati, kata inakuwa na kituo cha afya, wilaya kuwa na hospitali na ngazi ya mkoa na kanda kupata hospitali za rufani.

Hadi kufika Machi mwaka jana, takwimu za kibunge zilieleza hospitali za serikali jumla yake zilikuwa 202, ilhali kabla ya hapo Juni 2021, zilikuwapo 185. Hapo kuna maana ya ongezeko la hospitali 22.

Zingine na idadi ya awali kwenye mabano ni, vituo vya afya 679 (za mwaka 2021 ni 645), na zahanati 5491 zilikuwa 5491 kutoka 5395 za Juni 2021.

Kinachotokea sasa ni ishara ya mfano wa mwendelezo wa kazi za Rais Dk. Samia katika huduma za jamii akitekeleza MMAM, tafsiri ya nyongeza hiyo ni katika vituo vya afya, zahanati na hospitali kwa hitaji la ziada ya nguvukazi kupahudumia.

Hilo ndilo linakamilisha mahitaji ya wananchi mahali waliko katika kuzipata huduma mbalimbali, ikiwamo hiyo nyeti ya afya.

Ndani ya mustakabali huohuo, kumefunguliwa upana penye sekta ya elimu, ambayo tangu zama za uongozi wa nchi awamu ya tatu, kuna Mpango wa Mandeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES), vikishughulikia ngazi ya shule, nayo zao lake kukidhi mahitaji yaliyoko ndio sasa kuna mchakato wa ajira hizo, 21,200.

Huduma tajwa kwa ujumla ziko chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (Tamisemi), huku katika ngazi ya kisera, sekta hizo ziko chini ya wizara za Afya na Elimu.

**TAFSIRI YAKE**

Mara moja, alichoamua Rais kinatarajiwa kuboresha huduma tajwa za elimu na afya nchini, zao lake ni kubadilisha kiwango cha maisha ya Watanzania, ikizingatiwa MMAM, MEM na MMES, vyote kwa pamoja vinalenga tija katika upatikanaji huduma zake ikiwamo suala la umbali, hali kadhalika ubora wa maudhui inapotoa huduma husika, iwe afya au elimu.

Penye mafaniko ya mikakati inayoendelezwa na Rais Dk. Samia kwa sasa, inatajwa kufungua mlango mwingine wa kuibadili kiwango cha nchi, kupiga hatua zaidi kwa mujibu wa vigezo vya kimataifa.

Ni mtiririko wa maamuzi kukamilisha mkakati ya kisera anayoifanya kukishuhudiwa tayari katika upande wa kimataifa kukitoka taarifa mbalimbali za kufafanua nyendo za nchi kisiasa kwamba ni 'patulivu' kwa ajili ya kuwekeza na baadi ya benki zilizoondoka nchini, zimesharudi sokoni na zimeshaanza kazi.

Mbali na ajira za walimu na kada ya afya, pia ni kipindi kifupi kilichopita, Rais amewezesha kutangazwa ajira nyingi za Jeshi la Polisi hivi karibuni, ambazo mchakato wa uteuzi wake unaendelea hadi sasa, ikiwa na sera ileile ya awali ya nadharia ya kiuchumi, taifa kupata nguvu kazi itakayozalisha huduma zaidi kiusalama, ikiwa nayo ni kiashiria cha maisha bora.

**KAMA 'ZAMA ZILE'**

Ni mfumo wa maboresho ya maisha yaliyopo kimataifa. Kwa taifa jipya au kongwe elimu na afya, ni maeneo ambayo kila taifa linawekeza kwa kiasi kikubwa kwa umma wake, ikitoa zao la maendeleo.

Kada hiyo ya kijamii inapopata uelewa na ujuzi, basi inapata mageuzi makubwa na hasa kutumikia miundombinu na mazimgira walio nayo, rasmi na si rasmi.

Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, katika Mpango wa Muda Mfupi wa miaka mitatu mara baada ya uhuru na baadaye katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Nchi, 1964 hadi 1969, katika baadi ya sehemu kulikowekezwa sana ni katika elimu, kufumbua macho umma na wakati huohuo, kupata kada ya wataalamu mbalimbali kitaifa, huku sekta za afya na elimu zikiwa kwenye historia ya kipaumbele.

INAENDELEA UK. 12

# CAG alivyogonga hodi kwa Msajili, vyama vya siasa akikuta 'madudu'



Viongozi wa vyama vya siasa, wakiwa mkutanoni. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

**Na Sabato Kasika**

MNAMO Machi 29 mwaka huu, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Charles Kichere na ile ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Katika ripoti hiyo ya mwaka fedha wa 2021/22 iliyowasilishwa bungeni hivi karibuni, inaonyesha kuwapo uzembe katika usimamizi wa mali za umma kwa baadhi ya watendaji wa serikalki.

Ni ripoti hiyo iligusa maeneo mengi ambako kwa ujumla CAG na TAKUKURU zilibaini upotevu wa mabilioni ya fedha za umma. Zote mbili zilionyesha kuwapo 'upigaji' fedha za umma unaofanyika kwa uzembe au kwa namna nyingine na inawezekana kuchangia kukwamisha maendeleo ya nchi.

Ubadhirifu huo unatajwa umesababisha kuwapo mjadala mpana kutoka kwa watu wa kada mbalimbali, wakiwamo wanasiasa wanaotaka hatua za kisheria zichukuliwe kwa wote waliohusika na ubadhirifu huo.

Wakati umma unajadili upotevu huo, pia kwa upande wa vyama vya siasa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, ambao ni kama haujajadiliwa kwa kina, ingawa ripoti ya CAG imekuta kuna 'madudu'.

### HALI KATIKA VYAMA

Ripoti ya CAG inabaini kuwapo dosari katika uendeshaji vyama vya siasa, kukitajwa jumla ya vyama tisa vimebainika kushindwa kukusanya mapato yake na kuishia kukusanya asilimia 67 tu.

> Katika ufafanuzi wake, CAG anasema kwamba vyama vya UMD na UPDP vilishindwa kuhuisha madaftari hayo kwa miaka miwili mfululizo, kwa mwaka wa fedha wa 2020/21 na 2021/22.



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Charles Kichere.

CAG katika ripoti yake hiyo, anataja baadhi ya vyama hivyo kuwa ni CHADEMA, CUF, CCM, NCCR-Mageuzi, CHAUMMA, ADC, TLP, SAU na Demokrasia Makini na kwamba vilishindwa kukusanya mapato ya jumla Sh. bilini 25.85 katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Anaeleza kwamba katika mapitio ya bajeti ya vyama vya siasa, kukagua taratibu zilizotumika kuandaa, pamoja na kujumuisha bajeti hizo kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa shughuli za kisiasa za vyama hivyo, vilikuwa vimejiwekea malengo ya kukusanya mapato ya Sh. bilioni 78.75 kwa mwaka wa fedha 2021/22, lakini vikaishia kukusanya Sh. bilioni 52.90 tu.

Vilevile, CAG anabainisha kwamba, kuna vyama vinne ambavyo ni SAU, NCCR-Mageuzi, TLP na ADC, vilkudanya fedha chini ya asilimia 10 ya mapato yaliyokuwa yamewekwa kwenye bajeti zake na hapo mkaguzi huyo wa nchi, analitaja kuwa ni tatizo kubwa, ambalo ni vyema likashughulikiwa inavyopaswa.

Ripoti, pia inataja sababu za wanachama wake kushindwa kulipa ada zao za uanachama kwa kila mwezi, akinena kuwa ni kukosekana rejista za uanachama ni kukosa taarifa sahihi za wanachama, kwa kuwa hakuna utaratibu stahiki za ufuatiliaji huo.

Aidha, ripoti hiyo inaigusa CCM kuwa imenunua vitu visivyotumika vya Sh. milioni 58.60 vilivyopitwa na wakati na kwamba mabadiliko ya haraka ya kiteknolojia, havitumiki, huku menejimenti ya CCM ikitoa majibu kwamba vitu hivyo ni nyeti, vinasubiri kibali kutoka Bodi ya Wadhamini kwa ajili ya kuviharibu. Hakuvifafanua.

### TAARIFA ZA KICHAMA

Kwa mujibu wa CAG, Sheria ya Vyama vya Siasa, inavielekeza vyama vya siasa vilivyosajiliwa kutunza daftari ya viongozi na wanachama wake katika kila ngazi.

Hata hivyo CAG katika ukaguzi wake, anabaini baadhi ya vyama vya siasa kama DP, UMD, UPDP, ADA-TADEA na NRA, vimeshindwa kuhuisha madaftari ya taarufa za viongozi na wanachama wake.

Katika ufafanuzi wake, CAG anasema kwamba vyama vya UMD na UPDP vilishindwa kuhuisha madaftari hayo kwa miaka miwili mfululizo, kwa mwaka wa fedha wa 2020/21 na 2021/22.

Pia, kutokana na mazingira hayo, CAG anavishauri vyama vya siasa kuhuisha madaftari yenye kumbukumbu za taarifa za viongozi na wanachama kwa kutumia kanzidata za kielektroniki, ili kuwa na taarifa sahihi wakati wote.

Anashauri kitaalamu kuwa, hiyo ni hatua inayoweza kusaidia kuwapo kwa ufuatiliaji imara wa ada zisizolipwa, pia kuboresha ukusanyaji wa mapato na kuongeza ufanisi wa shughuli mbalimbali na mipango ya vyama hivyo.

### MSAJILI ALIVYOGUSWA

Ripoti ya CAG inafafanua kuwa pamoja na kuwapo kwa mapungufu kwenye baadhi ya vyama, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, haijaviwajibisha vyama vilivyoshindwa kuwasilisha madaftari yenye taarifa za wanachama.

Anasema kitendo cha kutowasilisha madaftari hayo, kinasababisha kuwapo kwa taarifa zisizo sahihi za idadi ya wanachama wa vyama hivyo na kwamba taarifa zinazohusiana na wanachama ni takwa la kisheria.

Kimsingi, ukaguzi unaofanywa na CAG ndani ya miundombinu ya kisiasa ni takwa na kisheria, mbali lnapata kungwa mkono na Rais Dk. Samia, kufanya ukaguzi wa hesab na mali za umma, ikiweka mazingira ya haki na uwajibikaji wa mali ya umma.

Tafsiri ya jumla ni kwamba, kuna haja ya kila upande ukatimiza wajibu wake, kuanzia na watendaji wa kiserikali, viongozi wa vyama vya siasa na wahusika wa kada nyinginezo.

## Uwekezaji wa Samia katika nguvukazi ya maelfu na ishara

**INATOKA UK. 11**

Walimu na wataalamu wa afya wengi waliandaliwa, huku serikali ikitafuta nafasi nyingi za kujiendeleza kimasomo wote kwa pamoja, hadi unatimia mpango huo mwaka 1969, zao la uwekezaji katika elimu lilionyesha mapinduzi makubwa, kuhusu kuboreka maisha ya umma.

Kuwapo vyuo na shule nyingi na zahanati, maana yake ni hitaji la walimu na watumishi kada ya afya wa ziada, huku kwenye radio ambayo ilikuwa mawasiliano makuu na nyenzo nyingine mbalimbali kukaendelezwa elimu ya umma.

Katika lugha rahisi, uwekezaji katika nguvu kazi iliyoelimika ni sehemu muhimu ya mafanikio ya Mpango wa Maendeleo wa Kwanza wa Mwaka 1964 hadi 1969 na mingine iliyofuata, leo hii Rais Dk. Samia akiwa zao la uwekezaji huo tangu awamu ya kwanza, anaendeleza umuhimu huo katika Serikali Awamu ya Sita.

# Mapigano moto Sudan, jirani Kusini, Kenya na Djibouti wajitosa usuluhishi

• Vifo vya watu vyagusa mahesabu ya mamia

**Na Mwandishi Wetu**

HALI ya amani nchini Sudan si shwari hata kidogo, usalama uko matatani, kukiripotiwa wastani wa watu 100 wameshakufa ndani ya siku hizo chache, huku juzi kukiwapo hesabu inayofikia 180.

Ni mazingira yanayolazimisha uamuzi wa haraka kutaka usuluhishi kupitia kikao cha haraka kinachofanywa na Jumuiya ya Igad, ambayo inaundwa na nchi nane za ukanda wa Pembe ya Afrika, Ukanda wa Mto Nile na Maziwa Makuu.

Huo ni muungano ulioko tangu mwaka 1986, unaojumuisha nchi ya Djibouti penye makao makuu, pia Ethiopia, Somalia, Eritrea, Sudan Kusini, Kenya na Uganda.

Jumapili iliyopita, viongozi wake waliendesha vikao vya mtandao, kupanga kutuma marais kutoka Kenya, Sudan Kusini na Djibouti, kwenda Sudan haraka iwezekanavyo, kupatanisha makundi ya kijeshi yanayopigana.

Pia, ikatoa wito wa kusitishwa mara moja, kwa uhasama kati ya pande zinazozana nchini Sudan. Hiyo inachuka nafasi, uwanja wa ndege wa kimataifa ukiwa umefungwa, hakuna uhakika kuwapo mpango wowote wa amani unaoweza kufanyika.

Kinachoendelea sasa Sudan, ni kuwapo mapigano kati ya vikosi vya serikali na wanamgambo cha RSF, yanayoendelea, licha ya kuwapo maombi ya jumuiya ya kimataifa, kwa pande zinazozozana kusitisha mapigano.

Rais wa Kenya, William Ruto, amewaomba viongozi wa Igad kuchukua msimamo wa kurejesha amani jijini Khartoum, huku Shirika la Chakula Duniani (FAO), limesitisha kazi yake baada ya wafanyakazi wake watatu kuuawa, huku ndege ya Umoja wa Mataifa ikiharibiwa vibaya.

**MZIZI WA MZOZO**

Hadi sasa kuna vyanzo kadhaa vinatajwa, huku mapigano yanayoendelea sasa, inaelezwa ni sehemu ya mzozo wa pande mbili ikihusisha kugombea udhibiti wa maeneo muhimu ya mji mkuu, Khartoum.

Kinachoendelea, kikosi cha Rapid Support Forces Paramilitary (RFS), kinasema kimechukua udhibiti wa Ikulu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa, madai ambayo bado hayajathibitishwa.

RSF hadi sasa inadai kukamata wanajeshi wa jeshi la Sudan na kuteka baadhi ya maeneo katika majimbo mengine nchini humo.

Kwa upande wake, jeshi la nchi hiyo linasema bado linadhibiti vituo vyote na viwanja vya ndege na jeshi la anga, huku linaendesha operesheni kukabiliana na RSF.

Madai ya kushambuliana pia yamekuwa yakichukua sura katika staili ya pande mbili, hazikubaliana kuhusu ukweli wa yule aliyeanzisha, kwani RSF inalishutumu jeshi kwa kuanzisha mapigano hayo, kwa kushambulia makao yake makuu mjini Khartoum na kuzingira, wanajeshi wa RSF waliokuwa hapo.

Lakini, jeshi la Sudan linasema



Jenerali Mohammed Dagalo (katikati) na kulia kwake ni Mwenyekiti wa Baraza la Sudan, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan. **PICHA: MTANDAO**

> “ RSF imeundwa mwaka wa 2013 ikiwa na wapiganaji wengi kutoka kwa wanamgambo wa Janjaweed, ambao walipigana dhidi ya waasi nchini Darfur.

kuwa RSF ilianza mapigano kwa kushambulia vyama vya kiraia vya Sudan, ambavyo vimetia saini makubaliano ya awali kugawana madaraka.

Hapo awali, RSF ilitoa wito kwa pande zote mbili kusitisha uhasama, pia ikatoa wito kimataifa na kikanda kuingilia kati na kusaidia haraka kukomesha umwagaji damu.

**HISTORIA ILOKOTOKA**

Tangu kutokea mapinduzi ya Oktoba 2021, Sudan imekuwa ikiendeshwa na Baraza la Majenerali na kuna wanajeshi wawili; Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, ambao tofauti kati yao ndio ikazua mzozo.

Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, ambaye ni mkuu wa majeshi na rais wa nchi hiyo kwa sasa na naibu wake, kiongozi wa RSF, Jenerali Mohamed Hamdan Dagalo, anayejulikana zaidi kama Hemedti.

Hawakubaliani na mwelekeo ambao nchi inaenda na hatua inayopendekezwa kuelekea utawala wa kiraia.

Ni ghasia 6ya zao la mvutano siku kadhaa, huku kikosi cha RSF kikisambazwa tena nchini kote, katika hatua ambayo jeshi inaona ni tishio kwao kitaifa.

Hadi sasa katika hatua ya kuibuka sakata hilo, haijabainika aliyefyatua risasi ya kwanza asubihi, Jumamosi iliyopita, lakini kunatajwa kuwapo hofu kwamba, hali hii itazidi kuwa mbaya zaidi.Wanadiplomasia nao wanazitaka pande hizo mbili kusitisha mapigano.

Mapigano katika hatua iliyopita, hata kuondolewa madarakani mwaka wa 2019, ni kwa Rais Omar al-Bashir aliyehudumu kwa muda mrefu ilianza na maandamano makubwa ya kupinga utawala wake uliodumu kwa wastani miongo mitatu, jeshi likaanzisha mapinduzi, hadi hatua ya kumuondoa madarakani.

Raia nao wakaendelea kudai nafasi katika mpango wa kuelekea kufikia utawala wa kidemokrasia, hata mpango mkakati wa kurejesha mamlaka mikononi mwa raia ulikubaliwa, Desemba mwaka jana. Lakini, mazungumzo ya kukamilisha hatua hiyo hadi sasa yamekwama.

Serikali ya pamoja ya kijeshi na ya kiraia ilianzishwa wakati huo, kisha ikapinduliwa katika mapinduzi mnamo Oktoba 2021 na tangu wakati huo, kunaelezwa ushindani kati ya Jenerali Burhan na Jenerali Dagalo umekuw juu zaidi.

Kikosi cha wanajeshi wa Rapid Support Forces (RSF) kimejitokeza kwa kujulikana na sifa mbaya, kikiwa katikati ya mzozo ambao ukishikwa na hoja za dai la kuelekea utawala wa kiraia.

Hapo kunaongozwa na Jenerali Mohamed Hamdan Dagalo, naibu kiongozi wa nchi akishutumiwa kwa ukiukaji wa haki za binadamu, ikiwamo mauaji yaliyotokea Juni 2019, ikiwagusa waandamanaji wasiopungua 120, walipofika katika makao makuu ya jeshi.

RSF imeundwa mwaka wa 2013 ikiwa na wapiganaji wengi kutoka kwa wanamgambo wa Janjaweed, ambao walipigana dhidi ya waasi nchini Darfur.

Mnamo mwaka wa 2015, wanachama wake 40,000 pia wakajiunga na muungano wa kijeshi ulioongozwa na Saudi Arabia, katika vita nchini Yemen na kuna wakati wakaetumwa kupigana nchini Libya.

Ili kuwezesha pendekezo la mpito kwa utawala wa kiraia, kulikuwapo mpango wa kuanza kuiunganisha RSF katika jeshi, lakini mzozano kati ya Jenerali Dagolo na Mkuu wa Jeshi, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, kuhusu ratiba ya mabadiliko hayo na nani angeongoza kikosi kipya, ni suala ambalo limejitokeza kuwa chanzo cha mzozo wa sasa.

Ni mvutano uliosambaa hadi kuzuka mapigano yaliyopoa ndani ya wiki iliyopo sasa. Hapo ukaanza kwa Jenerali Mohamed Dagalo na Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, ambao wamekuwa wakiiendesha nchi tangu Oktoba, mwaka 2021.

Pendekezo la kuhamia serikali inayoongozwa na raia linatjwa kukiuka ratiba ya kuunganisha RSF katika jeshi la taifa. Hata hivyo, RSF inataka kuchelewesha hatua hiyo kwa miaka 10, lakini jeshi likawa na wazo pinzani.

**MWELEKEO ULIVYO**

Inaelezwa sasa iwapo mapigano tajwa yataendelea kuwapo, basi yanaweza kusambaratisha nchi na kuzidisha machafuko ya kisiasa kwa hatua mbaya zaidi.

Wanadiplomasia wamekuwa na jukumu muhimu katika kujaribu kuhimiza kurejea utawala wa kiraia, ikitajwa watakuwa na shauku ya kutafuta njia kupata majenerali hao wawili kuzungumza, kama mtazamo wa awali unaoonekana kutoka nchi za Igad.

Pia, inatajwa ni fikra inayowashika wasudan wa kawaida, katika kufikia muafaka wa suala hilo.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Mkumbuke aliyekuwa Katibu Mkuu wa UN, pia Rais Dk. Kurt Waldheim



Wa katikati, kipindi alikuwa Ofisa wa Jeshi.

**Na Mwandishi Wetu**

KWA maisha ya zama hizo hadi kufika mwanzoni mwa miaka ya 1970, jina Kurt Waldheim, lilitikisa mno. Alikuwa Katibu Mkuu wa Nne wa Umoja wa Mataifa akidumu kutoka mwaka 1972 hadi 1981, huku baadaye akichukua kiatu cha kuongoza nchi yake Austria.

Pia, inapotajwa katika majina au orodha ya askari wenye alama katika Vita Kuu ya Pili ya Dunia, naye yumo akiunda mjadala ndani ya siasa za nchi yake, zikiwa na mvuto hadi kimataifa kutokana na kunguruma kwa nchi yake wakati huo.

Baada ya kushindwa katika kinyang'anyiro cha kusaka urais wa Austria, Waldheim aliingia katika kusaka nafasi kwenye Umoja wa Mataifa, ambako alikuwa akiungwa mkono na Urusi, kwa maana ya USSR.

Katika mizunguko miwili ya kwanza ya kuwania ukatibu mkuu Umoja wa Mataifa, mambo hayakumwia rahisi, alipata uungwaji mkono, pia akipingwa na China, Uingereza na Marekani.

Katika mzunguko wa tatu wa uchaguzi wa kumpata Katibu Mkuu wa UN, Waldheim akashinda, baada ya wajumbe wa kudumu wa UN waliposhindwa kukubaliana kutumia kura ya Veto. Waldheim alikalia kiti kilichoachwa na U Thant, kuanzia mwaka 1972 na akatoka mwaka 1981.

Baada ya kutoka, ndiko kukasikika simulizi huenda nafasi hiyo ingeshikwa na mwanadiplomasi wa Kitanzania, Salim Ahmed Salim, lakini simulizi zake ndefu, hazikufanikiwa kutokana na vkiwazo vua siasa kimataifa wakati huo.

> “Mwaka 1994, pia Papa Yohana Paulo II, alimtunuku Pian Order ambayo iliasisiwa na Papa Pius IX miaka ya 1560, kwa ajili ya kutambua mchango na uaminifu wake katika Kanisa Katoliki.



Dk. Kurt Waldheim, alipokuwa Katibu Mkuu Umoja wa Mataifa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**ALIKOTOKEA**

Mzaliwa huyo wa mwaka 1918, anasimulia katika rekodi ya maelezo yake kwamba, mapema mwaka 1941, Waldheim alikuwa miongoni mwa maofisa wa Kinazi katika Kikosi cha Mashariki, alikoongoza mapambano.

Desemba 1942 alijeruhiwa katika vita hivyo na ndipo huduma yake katika majeshi muungano ndani ya jeshi la Nazi au 'Wehrmacht' kutoka mwaka 1942 hadi 1945. Hilo ndilo likawa mjadala mkuu wakati akiwania urais wa Austria mwaka 1985.

Katika autobaiografia yake anasema, aliondolewa kuongoza kikosi hicho cha kijeshi katika mstari wa mbele hadi mwishoni mwa vita hivyo. Hapo ndipo akapopata fursa mbadala ya kwenda kusoma masuala ya sheria katika Chuo Kikuu cha Vienna, Austria wakati huo akiwa ameoa.

Baada ya kuchapishwa kwa autobiographia ake katika harakati hizo za kisiasa, nyaraka na ushahidi ulionekana kuwa huduma yake katika jeshi iliendelea hadi mwaka 1945 ambao akapandishwa cheo na kuwakatika nafasi ya uteni akiwa jeshini katika vituo vya kazi nchini, Ujerumani Austria na Uswisi.

Baada ya kumalzia kutumikia ukatibu mkuu wa Umoja wa Mataifa mwaka 1985 akajtosa kwenye kinyang'anyiro cha urais wa Austria, baada ya kushindwa katika awamu ya kwanza mwaka 1971.

Wakati wa kampeni zake, akajikuta tena pagumu wapizani wake wakitumia historia yake jeshini, kwamba alikuwa kwenye rekodi na historia wa askari katika Vita vya Pili vya Dunia huko walioitwa mwamvuli wa Nazi, wakimuunga mkono Dikteta Adolf Hitler. Hata hivyo, akapita kuwa Rais, kati ya mwaka 1986 hadi 1992 akiwa Rais na kabla ya hapo alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje.

Mnamo Juni 14, 2007 alifariki dunia mwanasiasa huyo na mwanadiplomasia wa Austria, akiwa na umri wa miaka 88. Alizaliwa Desemba 21, 1918 huko Sankt Andrä-Wördern, Austria, kutokana na maradhi ya moyo na mazishi yake yalifanyika Juni 23 mwaka huo huo, katika Kanisa la Stephen na alizikwa katika makaburi ya Marais wa taifa hilo.

Kimsingi, ni kanisa ambalo baada ya kumaliza kuhuidumu urais, mwaka 1992 likampa nafasi ya Mjumbe wa Heshima, ambayo hupewa mwanafunzi wa Kanisa la Roman Katoliki.

Mwaka 1994, pia Papa Yohana Paulo II, alimtunuku Pian Order ambayo iliasisiwa na Papa Pius IX miaka ya 1560, kwa ajili ya kutambua mchango na uaminifu wake katika Kanisa Katoliki.

**NYAYO ZAKE**

Mwaka 1944 tayari alishakuwa na shahada ya falsafa, katika eneo lake la kitaaluma la Sheria na ilipofika mwaka 1945, alishazama katika majukumu ya kidiplomasia na hadi kufika mwaka 1956, kaanza kutumia ngazi ya uwaziri wa nchi yake na diplomsia ngazi ya juu, ndio maana ilipofika mwaka 1971 akawa na 'jeuri' ya kuwania urais wakati huo, akaukosa.

Mwaka uliofuatia akaibukia kuwania ukatibu mkuu wa Umoja wa Mataifa, akaupata, hata kutumikia hadi mwaka 1981, akitenda mengi ya matokeo chanya na kihistoroa wakati huo dunia imeelemewa migogoro, ikiwamo usuluhishi wa siasa za Mashariki ya Kati .



## Taasisi yahimiza matumizi chanjo za ndani mifugo

**Na Elisante John,** SINGIDA

TAASISI ya Chanjo ya Mifugo Tanzania (TVI) iliyoko Kibaha mkoani Pwani, imewataka wafugaji, kutumia chanjo inayotengenezwa na viwanda vya ndani, ili kukabiliana na vita ya kiuchumi, yenye lengo la kupunguza wingi wa mifugo.

Meneja wa TVI, iliyo chini ya Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Dk, Charles Mayenga, alisema hayo juzi mkoani hapa juu ya uwapo wa chanjo bandia ya matone (TEMEVAC 1-2) ya kumkinga kuku dhidi ya ugonjwa wa mdondo.

Dk. Mayenga alikutana na wafugaji, wataalamu, wafanyabiashara na wamiliki wa maduka ya pembejeo za mifugo kwenye ukumbi wa chuo cha VETA mjini hapa ili kuwapatia elimu ya namna ya kuitambua chanjo bandia ya TEMEVAC 1-2.

Mtaalamu huyo kutoka TVLA inayomiliki kiwanda cha serikali cha kutengeneza chanjo ya mifugo, kilichoko Kibaha mkoani Pwani, alisema kuna baadhi ya watu wameingiza nchini chanjo hiyo ili kuhujumu soko la kuku wa Singida.

"Kama mnakumbuka, chanjo ya matone ilifanyiwa utafiti hapa Singida na imefanikiwa katika kudhibiti ugonjwa wa mdondo au kideri kwa kuku... sasa hivi ipo dawa kama hiyo, inafanana na inayozalishwa na kiwanda cha serikali," alisema.

Dk.Mayenga aliwataka washiriki kuwa makini na chanjo hiyo, kutokana na mwonekano wake ulivyo kwa macho ukionesha maandishi yakiwa hayasomeki vizuri, wakati ile ya serikali yapo kwenye mpangilio mzuri na yanasomeka vyema.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo, mmiliki wa duka la dawa, Dk. William Mafwere na Ester Munuo, walipongeza juhudi za serikali kwa kuwapatia elimu ya kutambua chanjo hiyo feki, jambo litakalolinda kazi zao na za wafugaji pia.

TVLA hutengeneza aina saba za chanjo, ikiwamo ya mdondo/kideri (TEMEVAC), homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP), homa ya mapafu ya mbuzi (CCPP), Kimeta (Anthrax), kimeta na chambavu (Tecoblax), chambavu (Blackquarer) na kutupa mimba (Brucellosis5-19.

# JKT kuzalisha tani 1,500 mbegu alizeti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limejipanga kuzalisha tani 1,300 hadi 1,500 za mbegu ya alizeti aina ya Records kwa ajili ya kuzigawa kwa wakulima katika maeneo mbalimbali ili kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula na kukabili uhaba uliopo sasa.

Pia JKT imejipanga kushirikiana na serikali kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kula nchini kwa kuzalisha mbegu za michikichi katika vikosi vyake mbalimbali.

Mkurugenzi wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa JKT, Kanali Peter Lushika, alisema hayo jana wakati wa kutembelea shamba la alizeti lililoko kijiji cha Chenene, chini ya kikosi cha JKT Makutupora mkoani hapa.

Kanali Lushika alisema katika mpango wa mwaka 2022/23, jeshi hilo limejipanga wamejipanga kulima ekari takribani 1,700 za mbegu za alizeti aina Recods katika vikosi mbalimbali ambayo imefanyiwa utafiti nchini na kuonyesha inatoa mafuta mengi.

"JKT imejipanga kuhakikisha inazalisha mbegu za alizeti aina ya Records kwa wingi hapa nchini lengo ikiwa ni kuzitawanya kwa wakulima ili kufanya kilimo chenye tija," alisema.

Pia alisema wameamua kuzalisha mbegu aina hiyo kwa sababu ina gharama nafuu katika upatikanaji lakini pia imefanyiwa utafiti na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Ilonga, Kilosa na kuonyesha hutoa kiasi kikubwa cha mafuta.

Hata hivyo, alisema kuna aina mbalimbali za mbegu za alizeti ambazo jeshi hilo limepanga kuzalisha lakini kipaumbele kikubwa ni aina hiyo kutokana na wakulima wengi wanaweza kuitumia na kuinunua kwa gharama nafuu.

"Mbegu hii itakapothibitishwa na Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu Tanzania (TOSCI) itaanza kutawanywa kwa wananchi kwa ajili ya kuanza kutumika," alisema Kanali Lushika.

Mkurugenzi huyo aliwahakikishia wakulima kupata mbegu bora kutoka JKT na kuongeza kuwa wakulima wajiandae kuendesha kilimo chenye tija kutokana na mbegu bora za alizeti ambazo zinazalishwa na jeshi hilo.

Alisema mpango wa JKT kwa mwaka 2023/24 ni kufungua mashamba makubwa ya mbegu za alizeti takribani ekari 5,000 ambazo zitakuwa na uwezo wa kuzalisha mbegu nyingi ambazo zitasaidia kutoa mafuta mengi ya kula.

Mkuu wa Utawala wa JKT, Brigedia Jenerali

Mabena, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa jeshi hilo, alisema wamejipanga kuhakikisha wanasaidiana na serikali kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kula nchini.

Jenerali Mabena alisema hivi sasa uhitaji wa mafuta ya kula nchini ni tani 650,000 lakini uwezo wa kuzalisha ni tani 290,000 ambapo alisema moja ya mikakati ya Jeshi hilo ni kuhakikisha wanazalisha kwa wingi alizeti na michikichi.

Alisema JKT kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, walikaa na kuamua jeshi hilo kulima mazao ya michikichi na alizeti katika vikosi vya jeshi hilo, lengo ikiwa ni kuzalisha mbegu kwa wingi ambazo zitasaidia wakulima kuzalisha kwa wingi mafuta.



Mkuu wa Tawi la Utawala la Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Brigedia Jenerali Hassan Mabena (kushoto), akikagua shamba la alizeti la kikosi cha JKT Makutupora katika kijiji cha Chenene, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma, alipotembelea shamba hilo jana. Kushoto kwake ni Kaimu Kamanda kikosi hicho, Meja James Macheta. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Serikali na Huawei zatiliana saini mkataba kupanua mkongo wa taifa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetia saini mkataba wa upanuzi wa mkongo wa taifa wa mawasiliano katika wilaya 23 nchini wenye urefu wa kilomita 1,520 utakaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 37 na utatekelezwa kwa miezi sita.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alibainisha hayo juzi kwenye hafla fupi ya utiaji saini kati ya Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL) na kampuni ya Huawei International.

"Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuhakikisha Tanzania inakuwa na miundombinu bora ya mawasiliano yenye kutumia teknolojia ya kisasa ambayo italeta tija na ufanisi katika kuongeza uzalishaji na ujenzi wa uchumi wetu na kuimarisha usalama na ulinzi wa taifa letu," alisema Nape. Pia alisema Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatambua matarajio makubwa waliyo nayo wananchi ya kufikishiwa huduma kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 -2025.

"Tunafahamu kuwa kuna juhudi kubwa ambazo zimefanywa na serikali kupitia wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ya kuimarisha sekta ya mawasiliano ikiwamo usimamizi wa mkongo wa taifa wa mawasilinao na kuhahakikisha unafika katika ngazi za mkoa, wilaya na katika mipaka ya nchi yetu," alisisitiza.

Alisema mikoa yote imeshaunganishwa katika mkongo na umefika katika vituo vya mipakani ambavyo vimepakana na nchi jirani, hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi muhimu katika ukanda wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Serikali kwa kutambua changamoto za wilaya zetu za kukosa mawasiliano ya uhakika ambayo yamesababisha wananchi katika wilaya hizo kukosa fursa mbalimbali za kijamii na kibiashara.

"Serikali imepanga kutekeleza mradi wa kuimarisha mawasiliano katika ngazi ya wilaya kwa kuunganisha wilaya zote kwenye mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa mawasiliano ambayo yatachochea maendeleo katika wilaya hizo na taifa kwa ujumla," alisema Nape

Waziri pia alisema kukamilika kwa mradi huo kutaleta mageuzi makubwa katika ukuaji wa maendeleo ya taifa.

"Mradi huu wa upanuzi wa mkongo wa taifa wa mawasiliano utasaidia kukuza matumizi ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) na kuongeza kasi ya upatikanaji wa intaneti yenye kasi. Mawasailiano yatasaidia wilaya kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato kwa kutumia mifumo ya kidijitali," alisema.

Pia alisema mawasiliano hayo yatasaidia serikali kufikisha utekelezaji wa Tanzania ya kidijitali hadi ngazi za wilaya na kwamba katika ngazi ya wilaya, yatafungua fursa kwa wananchi za kiuchumi kwa kuwa mawasiliano yatakuwa na uhakika.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Mhandisi Peter Ulanga, alisema mkataba huo uliotiwa saini unatakiwa kukamilika ndani ya miezi sita tangu kutiwa saini kwake.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutaondoa tatizo lililokuwapo awali la ukosefu wa mawasiliano katika wilaya hizo.



# Mzee afa kwa kukany'agwa na tembo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

Mkazi wa kijiji cha Igava, Mbarali mkoani Mbeya, Hamis Aloyce (75) amefariki dunia baada ya kukany'agwa na tembo.

Aloyce aliuawa April 16, mwaka huu, baada ya kuvamiwa na tembo huyo wakati akiendelea na shughuli zake za kilimo katika shamba lake la mpunga kijijini hapo.

Mwili wa Aloyce ulisafirishwa kwenda nyumbani kwao, Dodoma kwa ajili ya mazishi, na serikali iligharimia safari hiyo na shughuli zote za mazishi.

Akizungumza wakati wa kuaga mwili wa marehemu katika kijiji hicho, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwila, alisema baada ya kuvamiwa na tembo huyo, Aloyce alijeruhiwa vibaya na kwamba alipoteza maisha wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Mbarali.

Kanali Mwila, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, alitoa pole kwa familia na wakazi wa Igava kutokana na kifo cha mwenzao na kwamba gharama zote za mazishi zitagharamiwa na serikali.

"Tumefanya mawasiliano na askari wa wanyamapori kuweka kambi ili kukabiliana na uvamizi wa tembo ambao mara kwa mara wanaharibu mazao na kuua watu. Aidha, nawaomba wananchi mwendelee kutoa taarifa mkiona wanyamapori kwenye makazi yenu," alisema Kanali Mwila.

Diwani wa Igava, Sulleman Udesi, alisema suala la uvamizi wa tembo katika eneo lao limekuwa la kawaida kwa kuwa ndani ya mwezi mmoja, watu wawili wamepoteza maisha.

Alisema licha ya tembo kugharimu maisha ya watu na kuharibu mazao shambani kama vile mahindi na mpunga, hakuna hatua zilizochukuliwa na serikali kudhibiti uharibifu huo.

Udesi aliomba serikali kuchukua hatua za makusudi ili kusaidia wananchi kuishi kwa amani na utulivu kuliko ilivyo sasa kwamba maisha yao yamekuwa ya wasiwasi na kuhofia baa la njaa kwa sababu tembo hao huaribu eneo kubwa la mazao shambani.

Mwenyekiti wa kijiji cha Igava, Hamad Jumbe, alisema tangu aingie madarakani amekuwa akipata malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya uvamizi wa tembo kwenye makazi ya watu na shambani.

Ofisa Uhifadhi na Mkuu wa Hifadhi ya Ruaha- Ihefu Mashariki, Deogratius Mwageni, alisema katika kukabiliana na wanyama waharibifu katika eneo hilo wameanzisha kambi ambayo itazuia uvamizi wa tembo kwenye makazi ya wananchi.

Aliwaomba wananchi kuwa watulivu katika kipindi hiki kwa kutochukua hatua ikiwamo kuwauwa au kuwafukuza tembo hao badala yake watoe taarifa mapema pindi wanapovamiwa.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa (wa pili kulia), akishiriki futari iliyoandaliwa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson kupitia Taasisi yake ya Tulia Trust, wilayani humo juzi. Kulia ni Shekhe wa Mkoa wa Mbeya, Msafiri Njalambaha. **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

# Uongozi wakalia mil. 15/- ujenzi vyoo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

KAMATI ya Maendeleo ya Kata ya Kalobe katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya inatuhumiwa kukalia fedha zaidi ya Sh. milioni 15 ambazo zilitolewa na serikali kwa ajili ya Ujenzi wa Vyoo vya Shule ya Sekondari Kalobe.

Hatua hiyo imesababisha wanafunzi kuwa hatarini kupatwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na uhaba wa matundu ya vyoo shuleni hapo.

Mwezi uliopita, gazeti hili liliripoti uwapo wa hatari ya wanafunzi wa kike katika Shule ya Sekondari Kalobe, kupata magonjwa ya mlipuko baada ya vyoo walivyokuwa wakitumia kubomoka kutokana na mvua inayoendelea kunyesha mkoani Mbeya. Akizungumza na Nipashe, Kaimu Mkurugezi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Wakili Triphonia Kisiga, alisema halmashauri tayari imechukua hatua za kunusuru wanafunzi hao kwa kutoa fedha zaidi ya Sh. milioni 15 ili zitumike kujenga vyoo shuleni hapo.

Alisema fedha hizo zilitolewa mwezi uliopita na kuiingizwa kwenye akaunti ya Kamagti ya Maendeleo ya Kata ya Kalobe ili zipelekwa shuleni kuanza ujenzi wa vyoo hivyo, lakini anasikitika kuona mpaka sasa kazi ya ujenzi bado haijaanza.

"Halmashauri kwa kujali afya za wanafunzi wetu tumechukua hatua za haraka za kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyoo shuleni hapo kabla ya kutokea madhara. Tuliingiza fedha hizo kwenye akauti ya Kata ya Kalobe ili Kamati ya Maendeleo ya Kata isimamie kazi hiyo, lakini kinachonishangaza ni kwamba fedha hizo hazijaanza kutumika kama tulivyokusudia," alisema Wakili Kisiga. Alisema baada ya kuona fedha hizo zimekaliwa, ameagiza zitolewe mara moja kwenye akauti hiyo na kuingizwa kwenye akauti ya shule ili kazi hiyo sasa isimamiwe na mkuu wa shule.

Mkuu wa Shule ya Sekondari, Songa Halson, alisema baada ya kutokea kwa tukio hilo alitoa taarifa kwa bodi ya shule na kukubaliana kukatisha masomo kwa muda ili kulinda afya za watoto hao.

Alisema kikao kiliazimia shule isifungwe badala yake wanafunzi wa kike waendelee kutumia vyoo vya walimu wa kike matundu mawili kwa muda na kwamba tayari uchimbaji wa shimo kwa ajili ya vyoo vipya ulianza na ujenzi unaendelea.

"Baada ya tathmini kufanyika tulikubaliana kujenga vyoo vipya zaidi ya matundu 320 ambavyo gharama yake itakuwa Sh. milioni 69 mpaka kukamilika kwake na kwamba wataalam wametuahidi kuzingatia ubora ili tatizo hili lisijirudie tena," alisema.

Baada ya kupata taarifa ya vyoo vya shule kubomoka, Mbunge wa Mbeya Mjini ambaye pia ni Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, alitoa mifuko 100 ya saruji.

# Pori la Kipengere lawavutia watalii

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

PORI la Akiba la Mpanga Kipengere limekuwa kivutio kikubwa cha watalii kutoka ndani na nje ya nchi licha ya kutokuwa na wanyama wakubwa.

Ofisa Uhifadhi Wanyamapori, Upendo Kimaro, alisema uwapo wa maporomoko makubwa ya maji, Pango la Asili na la kihistoria la Chifu Mkwawa pamoja na bustani nzuri ya maua, vimekuwa sababu kubwa ya watu wengi kwenda kutembelea pori hilo.

Alisema Pori hilo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,574 limekuwa kivutio kwa watalii wengi katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini kutokana na mambo mengi yaliyomo na ambayo hayapatikani katika hifadhi zingine.

"Tunafurahia kuona mwitikio wa watalii kutembelea Mpanga Kipengere ni mkubwa. Kwa sasa tunapokea watalii wa ndani 30 hadi 50 kwa mwezi na wageni kati ya 15 na 20 idadi ambayo ni kubwa ukilinganisha na ilivyokuwa awali kabla hatujaanza kujitangaza," alisema Upendo.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha pori hilo linakuwa kivutio kikubwa ukanda wa Nyanda za Juu Kusini, wameanza kuboresha miundombinu ya barabara ili kusaidia watalii kufika bila vikwazo.

Pia alisema wamekamilisha ujenzi wa vyumba vya kulala watalii ambavyo vimezingatia mahitaji ya kila mtu kwa gharama nafuu ambayo inaendana na hali za maisha za watanzania na wageni.

Aliongeza kuwa licha kubarikiwa bustani nzuri ya maisha katika eneo la Ibaga na maporomoko ya maji ya Kimani, wanakabiliwa na tatizo la uvamizi wa majangili ambao huingiza mifugo yao ndani na wakati mwingine kujihusisha na shughuli za kilimo.

"Kuna mwingiliano wa wananchi kuchuma chikanda ambayo nchini Zambia ina soko kubwa kwani ndio chakula kikuu eneo hilo, tunaendelea na oparesheni za mara kwa mara kudhibiti hali hiyo na kutunza uoto wa asili uliopo," alisema Upendo.





## SMZ, wawekezaji kutatua kero ajira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kutoa ushirikiano kwa wawekezaji wazawa katika kukuza uchumi na ajira nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa duka kubwa la biashara ya nguo la mfanyabiashara mzawa, Fred Ngajiro, maarufu kama Vunja Bei), katika mtaa wa Raha Leo, Zanzibar.

Kitwana alisema serikali inahamasisha masuala ya uwekezaji, hivyo aliahidi kutoa kila aina ya ushirikiano kwa mfanyabiashara huyo mwenye nia ya kuwasadia Wazanzibari.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa, duka hilo limefunguliwa muda mwafaka katika kipindi ambacho wananchi wana mahitaji mengi kwa ajili ya Sikukuu ya Idd el Fitri.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Kitwana alisema duka hilo litatoa unafuu kwa wananchi wa Zanzibar. Pia alisema licha ya wananchi kupata huduma pia vijana watapata fursa ya ajira.

Alisema fursa hizo za ajira zitapunguza wimbi la vijana ambao wapo mitaani hawana ajira na wengine kujiingiza katika vitendo viovu ambavyo ni kinyume na maadili.

"Nampongeza sana mmiliki huyu kwa sababu hii ni moja ya juhudi za Rais wa Zanzibar (Dk. Hussein Ali Mwinyi) katika kukuza uwekezaji na upatikanaji wa huduma muhimu," alisema Kitwana.

Pia alisema uwapo wa duka hilo utapunguza msongamano wa wananchi kufuata huduma katika eneo la darajani.

Alisema anafarajika kuona bei za bidhaa katika duka hilo ni za kila rika hata wale wenye kipato cha chini wana uwezo wa kupata huduma.

Ngajiro aliipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na mkoa kwa mapokezi yao na kuruhusiwa kufanya uwekezaji huo ili kuwahudumia wananchi wa Zanzibar.

"Baada ya kuona wananchi wa Zanzibar wana uhitaji mkubwa wa kupata bidhaa zetu, tumeamua leo (jana) tuwafikie maana wakati mwingine wamekuwa wakisumbuka kutufuata Dar es Salaam," alisema.

Meneja Mauzo wa duka hilo, Adil Harold, alisema wamezingatia taratibu zote za ulinzi na usalama dukani hapo ili kunusuru vitendo vya kihalifu ambavyo vinaweza kutokea.

Pia alisema anasikitika sana kuona eneo hilo jalijazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu ambao nao ni sehemu ya wananchi wanaohitaji kupata biadhaa.

Alisema licha ya miundombinu kutokua rafiki, aliahidi kuwahudumia vizuri kundi hilo bila ya kutojali hali zao za kimaumbile.

# Wanawake bado wakumbana na vikwazo kufikia malengo uongozi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya jitihada zinazochukuliwa na taasisi zisizo za kiserikali katika kuwapa elimu wanawake kuwania nafasi katika vyama vya siasa, bado kuna changamoto kufikia malengo yao, imeelezwa.

Wakichangia katika mkutano wa asasi za kiraia na wahamasishaji jamii kwa ajili ya kujadili changamoto za uongozi na demokrasia ulioandaliwa na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) mjini hapa, wadau hao walisema bado kuna tatizo la kupewa nafasi kwa wanawake hasa katika vyama vya siasa. Hatua hiyo, wamesema ni kikwazo katika kufikia malengo yao.

Asha Aboud, mmoja wa wadau hao, alisema baadhi ya vyama vya siasa vimekuwa na mfumo ambao si rafiki kwa mwanamke hasa kupambana na mwanamume katika majimbo ya uchaguzi.

Kwa mujibu wa Asha, bado mfumo wa vyama vya siasa umetawaliwa na mfumo dume hali ambayo imesababisha wanawake kukosa nafasi za uongozi katika vyama hivyo.

Mwanaharakati huyo alisema katika kufikia mandeleo ya wanawake ni lazima kupewa nafasi ya kuingia katika sehemu za ngazi ya uamuzi katika uongozi ili kutatua changamoto zao ndani ya jamii.

Huda Gharibu Juma kutoka Jumuiya ya Kupambana na Changamoto za Vijana Zanzibar, alisema wanawake wengi wanapenda kujitokeza katika kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika vyama vya siasa lakini kuna changamoto ya upatikanaji wa tarifa kwa walengwa hao.

Alisema mazingira ya nafasi za uchaguzi kwa wanawake bado changomoto ikiwamo tatizo la umaskini wa kipato na rushwa ya ngono ndani ya baadhi ya vyama vya siasa.

Kwa mujibu wa Huda, mtoto wa kike anapozaliwa huwa haandaliwi kuwa kiongozi badala yake mtoto wa kiume hupewa nafasi zaidi katika kupangiwa mipango ya kuwa kiongozi wa baadaye jambo ambalo si sahihi.

Meneja Uendeshaji wa Umoja wa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, Donald Godwin, alisema wanawake wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto mara mbili zaidi ikilingnaishwa na wasio na ulemavu.

Alisema bado watu wenye ulemavu ni waathirika wa mambo mbalimbali katika kupata nafasi za uongozi ndani na nje ya vyama vya siasa.

Mratibu wa Mradi wa Kuongeza Ushiriki wa Wanawake katika Masuala ya Demokrasia kutoka ZAFELA, Khamis Ali Rashid, alisema lengo la mkutano huo ni kutoa fursa kwa wadau kujadili changamoto katika nafasi za uongozi kwa wanawake.

Alisema mradi huo umekuwa ukiwapa elimu wanawake juu ya kujitambua katika kugombea nafasi kwa vile wanawake wakipewa nafasi wanaweza na kuleta maendeleo.



Umati wa wananchi wa Zanzibar wakiwa wamepanga foleni kwa ajili ya kupata huduma ya kununua nguo katika duka la Vunja Bei, eneo la Rahaleo, kwa ajili ya maandalizi ya Sikukuu ya Eid Al Fitr. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

# Serikali yasikia kilio wasafiri majini

**Na Mwandishi Wetu**

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeamua kutengeneza meli ya MV Mapinduzi II ili kuwaondolea usumbufu wananchi wanaotumia usafiri wa baharini kati ya Unguja na Pemba.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed amesema hayo jana alipofanya ziara ya kukagua matengenezo ya meli hiyo ambayo kwa sasa iko nangani katika bandari ya Malindi, Zanzibar.

Waziri huyo alisema serikali imeamua kuchukua hatua hiyo kutokana na usumbufu wa usafiri unaowakabili wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba.

Alisema matengenezo hayo yalioanza Febuari, mwakah uu, yanahusisha matengenzo ya injini zote mbili za meli, majenereta mawili yaliyoharibika kutokana na kufa kwa mfumo wa upozaji wa maji.

Dk. Khalid alisema ameridhishwa na kazi inavyoendelea na kwamba hadi sasa sasa baadhi ya mifumo imeanza kufanya kazi ikiwamo wa mwangaza ambao umewezesha taa za meli kuanza kuwaka na kurudi katika hali yake.

"Mimi na wenzangu tumeridhishwa na kazi nzuri inavyoendelea kwani mafundi wanafanya kazi takribani saa 24," alisema.

Pamoja na kazi hiyo, Waziri amewashauri mafundi wanaofanya matengenezo kuagiza vifaa kwa wingi na kwa pamoja vitakavyowezesha meli hiyo kukamilika ndani ya kipindi cha makubaliano ya mkataba.

Kuhusu mkataba, Waziri Dk. Khalid alisema umetoa nafasi kwa mafundi hao kuendelea kubaki nchini kwa kipindi cha miaka miwili ili kuendesha meli hiyo wakiwa wanawafundisha watalamu wazalendo ili pindi watakapoondoka wawe na uwezo mzuri wa kuiendesha meli hiyo.

Mtendaji Mkuu wa Kookje Enginering kutoka Korea Kusini, Diy Kwak, alisema kazi hiyo inatarajiwa kukamilika Septemba, mwaka huu na kwa sasa inaendelea vizuri huku kampuni ikiendelea kuagiza vifaa.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAHMAN JUMA KASWAKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **VITZ SALOON** yenye usajili namba **T 188 BKU,** CHASSIS NAMBA: **SCP10032241Z** na ENGINE NAMBA: **1SZEAA2414**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **PWA/BAG/132499**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**STEVE JOHN MILANZI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI** yenye usajili namba **T543 DMA** , CHASSIS NAMBA: **MMBJNKB407D119939** na ENGINE NAMBA: **4D36UCAS2133**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/94732/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**

**Kituo cha Njombe Mjini, Mkoa wa Njombe**

**Usimamizi wa mirathi Na. 31/2023**

**JAMES MWAIKAMBO.....................Marehemu**

**BASILISA NZIKU...................Msimamizi**

**TAARIFA KWA WADAI**
**(Kanuni ya 9(1) ya Nyongeza ya V ya Sheria ya Mahakimu wa Mahakama Sura ya 11 Rejeo la 2019)**

TAARIFA inatolewa hapa kwa wote wanaodai kuwa na madai yanayohusiana na mali za marehemu, mtajwa hapo juu JAMES MWAIKAMBO, aliyefia Dar es salaam tarehe 05 mwezi wa 02 mwaka 2023 na Mahakama kunipa barua ya usimamizi wa mirathi hiyo BASILISA NZIKU siku ya tarehe 14 mwezi April mwaka 2023, hapa sasa wanatakiwa kunipa madai yao kwangu kupitia namba sanduku langu la barua Njombe au namba ya simu 0752205033 au kuniletea kwa binafsi, ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya kutangazwa taarifa hii ambapo muda wake utapoishia nitaendelea kukabidhi mali za marehemu kwa warithi wanaostahili, nikizingatia tu madai ambayo nitakuwa nimearifiwa.

MAHAKAMA YA MWANZO NJOMBE MJINI
WILAYA YA NJOMBE
17/04/2023
HAKIMU
NJOMBE - MJINI

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI NAMBA 35/2018**
**ALOYCE MAPOLE....................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**JULIUS WELLA**
**ROGATUS ANACLET MAPUNDA.........WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Wajibu maombi mnataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yenu. Hivyo basi mnatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wenu, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 20/04/2023 saa 2:30 asubuhi kusikiliza hukumu hapa Barazani.

Kumbuka pia kushindwa kwenu kufika shaurini kutapelekea Baraza hili kusoma hukumu upande mmoja bila kujali uwepo wenu.

Imetolewa leo name na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 14/04/2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SONGEA

TANZANIA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHARLES EDWARD NYANGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.469 DNW** yenye Engine No; **IJZ1247265,** Chasis No; **JCG100022117** aina ya **TOYOTA BREVIS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi. **BGA/RB/1457/2021.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MULEBA**
**LILILOPO MULEBA MKOA WA KAGERA**
**MAOMBI NA. 06/2023**
**ANASTELLA ATHANAEL ............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1. CONSOLATHA KANUNSHU**
**2. BRASIO ATHANAEL .........WAJIBU MAOMBI**

**KWA: 1. BRASIO ATHANAEL (POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa maombi Na. 06/2023 yamepangwa kutajwa tarehe 05.05.2023 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, J. K. Banturaki saa 2:30 asubuhi, mahali - Muleba (Mamlaka ya Mji Mdogo).

Hivyo, unaamriwa kuhudhuria mwenyewe wawakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza kesi upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 21.03.2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MULEBA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**

**MKOA WA MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MADAI NA. 1/2023**

**SHINBA-SAN LIMITED: .....................MDAI**

**DHIDI YA**

**YONA T. MATEMBO: .....................MDAIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**
**YONA T.MATEMBO**

**POPOTE ULIPO**

Unatakiwa ufike katika Mahakama ya Wilaya Morogoro tarehe 25/04/2023 saa 2:30 asubuhi ambapo shauri lako limepangwa kutajwa.

Endapo hutofika wewe binafsi ama mwakilishi wako shauri tajwa litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.

Imesainiwa leo tarehe 05 mwezi March mwaka 2023

E.B.USHACKY
HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MOROGORO.
RESIDENT MAGISTRATE INCHARGE
DISTRICT COURT
P. O Box 660, Morogoro

## KUPOTEA KWA CERTIFICATE

**SHAJI MICHAEL AREEPARAMPIL** anatangaza kupotea kwa CERTIFICATE OF REGISTRATION of THE DIVINE WORD MISSIONARIES TANZANIA yenye namba SO NO.13043 . Kwa atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi ARU/ARU/RB/81877/202**

**THE REGISTRATION OF DOCUMENT ACT**
**(CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

BY THIS DEED, I, NAHIDA ABDUL RAHIM of P.O. Box, DAR ES SALAAM, DO HEREBY wholly, absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former names of NAHIDA IBRAHIM HAMISI and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of my former name, the name of NAHIDA ABDUL RAHIM. The reason for the change of name is that when I got married I adopted the names of NAHIDA IBRAHIM HAMISI from my ex-husband but following following breakup it my wishes from now onward to adopt the names of NAHIDA ABDUL RAHIM as its 19660626-14113-00002-13. For the purpose of evidence such determination, I hereby DECLARE that I shall at all times hereinafter in all records, deed, documents and other writings and in all action, suits and proceedings as well as in all Public and Private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the said name of NAHIDA ABDUL RAHIM as my name in lieu of and in substitution for my former names of NAHIDA IBRAHIM HAMISI. AND I HEREBY expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated, describe and address me by the adopted name of NAHIDA ABDUL RAHIM.

IN WITNESS WHEREOF I have set my hand at Dar es salaam, and I hereon substitute my old names of NAHIDA IBRAHIM HAMISI by my new name of NAHIDA ABDUL RAHIM.

SIGNED and DELIVERED by the said NAHIDA ABDUL RAHIM who is known to me personally / identified to me by .................... the latter being known to me personally in my presence this ... day of ... 2023

DEPONENT

Name: ....
Signature: ....
Postal address: ....
Qualification: ....



## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SALEH OMAR AL- JABRY** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC393DTS aina ya SINORAY SMASH 110. Chassis No. LVVMXCHLP7M1002323, Engine No. 1P52FMH2H2H002323. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya polisi. **DOD/DOD/RB/128197/2023.**


# OFISI ZA MATANGAZO

## MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
## PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
## MOB: +255 - 0677020701
## E-mail: advertise@guardian.co.tz,
## Website: www.ippmedia.com


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA


# Rais Putin azuru Kherson, Bakhmut ikishambuliwa

**Kherson,** UKRAINE

RAIS wa Russia Vladimir Putin (pichani), ametembelea maeneo aliyoyachukua Ukraine katika mikoa miwili ikiwamo Kherson, huku vikosi vya Russia vikizidisha mashambulizi ya anga kwenye mji wa Bakhmut, mashariki mwa Ukraine.

Putin, pia alihudhuria mkutano wa kijeshi, ili kusikiliza ripoti kutoka kwa makamanda wa kijeshi na inadaiwa alitembelea eneo la Luhansk.

Russia, iliuchukua mji wa Kherson na Luhansk mwaka jana.



Safari kama hizo za kiongozi wa Russia ni nadra, ingawa alifanya ziara ya kushtukiza katika jiji la Mariupol, Machi, mwaka huu.

Haijulikani ni lini safari ya Kherson ilifanyika, huku vyombo vya habari vya Russia, vikiripoti kwamba, Rais Putin pia aliuliza kuhusu hali ilivyo katika eneo la Zaporizhzhia, ambako Moscow inadai kuwa sehemu ya Russia.

Alinukuliwa akizungumza katika mkutano wa kijeshi huko Kherson kwamba. "Ni muhimu kwangu kusikia maoni yako juu ya jinsi hali inavyoendelea, kuwasikiliza, kubadilishana taarifa," alisema.

Wanajeshi wa Russia, waliondoka kutoka mji wa Kherson mwishoni mwa mwaka jana na kupoteza mji mkuu pekee wa kikanda, ambao ilifanikiwa kuuteka tangu Russia ilipovamia Ukraine, Februari mwaka jana.

Hata hivyo, baadhi ya kanda bado ziko chini ya udhibiti wa Russia. **BBC/REUTERS**





Kamanda wa Vikosi vya Wanajeshi wa Sudan, Abdel Fattah al Burhan (kulia) na Kamanda wa Vikosi vya Wanamgambo wa Rapid Support Forces (RSF), Mohammed Hamdan Dagalo. **PICHA: BBC**

# Mapigano Sudan; takribani 200 wauawa, majeruhi 1,000

**KHARTOUM,** Sudan

KUNDI la wanamgambo la Sudan, Rapid Support Forces (RSF), limesema limesitisha mapigano kwa saa 24 ili kupisha misaada ya kiutu.

Msafara wa wanadiplomasia wa Marekani ulishambuliwa juzi, ingawa hakukuwa na majeruhi. Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alisema.

Blinken alizungumza na Kamanda wa Vikosi vya Wanajeshi wa Sudan, Abdel Fattah al Burhan na Kamanda wa Vikosi vya Wanamgambo wa Rapid Support Forces (RSF), Mohammed Hamdan Dagalo.

Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini Sudan, Aidan O'Hara, alishambuliwa nyumbani kwake mjini Khartoum, ambako kumekuwa na mapigano makali kati ya vikosi hivyo.

Hata hivyo, RSF limesema limesitisha mapigano kwa muda wa saa 24 zijazo, ikiwa ni njia moja ya kutoa nafasi kwa raia kupata misaada kwa njia salama.

Mkuu wa RSF, Dagalo, anayejulikana zaidi kama Hemedti, alisema makubaliano yamefikiwa, baada ya mazungumzo na Blinken na mataifa mengine rafiki.

"RSF inathibitisha tena kuidhinisha uwekaji silaha chini kwa muda wa saa 24, ili kuhakikisha kuwa raia wanapita salama na kuwahamisha waliojeruhiwa," Hemedti alisema.

Alilishutumu jeshi kwa kushindwa kuheshimu usitishwaji wa mapigano ya awali wa Umoja wa Mataifa (UN), akisema wanajeshi hao wanadaiwa kushambulia kutoka angani, maeneo yenye wakazi wengi na kuhatarisha maisha ya raia.

"Hatua hizi ni ukiukaji wa wazi wa misingi na kanuni za sheria za kimataifa na za kibinadamu," aliongeza.

Hata hivyo, Jeshi la Sudan limepuuzilia mbali madai ya wapiganaji wa kijeshi wa RSF, kuhusu makubaliano ya siku moja ya kusitisha mapigano na kudai kuwa hizo ni propaganda.

"Hatujui uratibu wowote na wapatanishi na jumuiya ya kimataifa kuhusu usitishaji vita na tangazo la waasi la usitishaji mapigano kwa saa 24, linalenga kuficha kushindwa ndani ya saa chache," Msemaji wa Jeshi la Sudan, alisema katika ukurasa wa Twitter wa Jeshi.

"Tumeingia katika hatua mbaya na juhudi zetu zinalenga katika kufikia malengo yake katika ngazi ya utendaji," taarifa ya jeshi iliongeza.

Wakazi katika mji mkuu wa Sudan, Khartoum wako kwenye hofu, huku mapigano ya bunduki na milipuko ya mabomu yakitikisa mitaa ya mji huo.

Ndege za kivita na helikopta za mashambulizi zilitanda angani na milio ya risasi ilisikika mjini humo, mapema jana asubuhi, huku miili ikisambaa mitaani na idadi ya waliofariki ikikaribia 200. **BBC**

# Macron atetea umri wa kustaafu kupanda

**Paris,** UFARANSA

RAIS wa Ufaransa Emmanuel Macron, ameyatetea mageuzi ya mfumo wa pensheni, akisisitiza kwamba kupandisha umri wa kustaafu nchini mwake ni hatua ya lazima, akisema uwe miaka 64.

Macron, alisema hayo katika hotuba aliyotoa kwa njia ya televisheni. Ameeleza kwamba ni lazima kupandisha umri wa kustaafu kutoka miaka 62 hadi 64, ili kuepusha kusambaratika kwa mfuko wa malipo ya uzeeni.



Hata hivyo rais huyo amekiri kuwa mageuzi hayo hayaungwi mkono na amesema anatambua kwamba wananchi wamekasirika.

Wanaoyapinga mabadiliko hayo nchini Ufaransa, walisema hotuba ya Rais Macron haikusaidia kupunguza mivutano na jumuiya za wafanyakazi zimeazimia kuendelea na maandamano ya kupinga mabadiliko hayo.

Wakati Rais Macron akitoa hotuba hiyo jana, waandamanaji waliendelea na harakati zao nchini Ufaransa kote. **DW**

# Merkel atuzwa kwa utumishi uliotukuka

**Berlin,** UJERUMANI

KANSELA wa zamani wa Ujerumani Angela Merkel, leo ametunukiwa nishani ya juu ya taifa, ambayo hutuzwa watu waliojitolea utumishi wa kutukuka kwa taifa.

Nishani hiyo itatoa nafasi kwa wafuatiliaji wa siasa za Ujerumani na umma wa taifa hilo, kutathmini kwa kina urathi wa kiongozi huyo wa zamani.

Hafla ya kutolewa nishani hiyo kwa Merkel, ilifanyika jioni jana, mjini Berlin na itakabidhiwa na Rais wa Shirikisho la Ujerumani Frank-Walter Steinmeier.

Rais wa Ujerumani kwa nafasi yake kama mkuu wa nchi anazo nishani lukuki, ambazo anaweza kuzitoa kwa raia waliojitolea utumishi wao kwa taifa.



Kwa mujibu wa ofisi ya Rais Steinmeier, nishani itakayotolewa kwa Merkel, ndiyo ya heshima zaidi kuliko nyingine.

Nishani hiyo iliyoanza kutolewa tangu mwaka 1951 hupewa raia wa Ujerumani na hata watu kutoka nje waliowezesha mafanikio ya kupigiwa mfano katika nyanja za siasa, uchumi, jamii na taaluma.

Merkel, anakuwa mwanamama, mwanasiasa wa tatu kutunukiwa nishani hiyo. **DW**

# RAIS SAMIA AMPONGEZA GEAY, AFUNGUKA MAZITO

Na Adam Fungamwango

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, amempongeza Mwanariadha Gabriel Geay, kwa kutwaa medali ya fedha, alipofanikiwa kukamata nafasi ya pili kwenye mbio za Boston Marathon zilizofanyika juzi nchini Marekani.

Katika salamu zake za pongezi juzi kupitia akaunti yake ya Instagram, baada ya kumalizika kwa mbio hizo, Rais Samia alimwambia mwanariadha huyo kuwa jitihada zake zimeijengea heshima nchi, akimtakia kila la kheri azidi kusonga mbele na mafanikio kwenye mchezo huo, huku akiahidi kuwa serikali itaendelea kuwaunga mkono wanamichezo.

"Nakupongeza Gabriel Gerald Geay kwa kuwa mshindi wa pili katika mashindano ya Riadha ya Kimataifa ya Boston yaliyofanyika leo [juzi] nchini Marekani. Jitihada zako zimeijengea heshima Tanzania. Nakutakia kheri katika kusonga mbele zaidi. Serikali itaendelea kuwaunga mkono wanamichezo," aliandika Rais Samia.

**Geay alimaliza mbio hizo akitumia muda wa saa 2:06:04, nyuma ya bingwa mtetezi, Mkenya Evans Chebet, aliyeshinda mara mbili mfululizo mashindano hayo, juzi akitumia saa 2:05:54.**

Akizungumza kutoka nchini Marekani, mwanariadha huyo alisema alikimbia mbio hizo akiwa amekunywa dawa ya kutuliza homa ambayo ilimshika tangu alipotua nchini humo.

"Tangu nilipotua hapa sikuwa kwenye hali nzuri, nadhani ni kutokana na hali ya hewa, nikapata homa na kabla ya kukimbia ilibidi nipate kwanza dawa ya kuituliza ili nikimbie vizuri na nimefanikiwa kwa hilo," alisema Geay.

Alisema siri ya kufanya vema ni maandalizi mazuri kuelekea kwenye mashindano hayo, ikiwamo kuwafahamu vema wapinzani wake aliokutana nao.

"Siri ya ushindi ni maandalizi mazuri na mazoezi kuelekea kwenye mashindano, nilikuwa na matumaini kwenye mbio hizi kuwa nitafanya vizuri na kilichokuwa kinanifanya kufikiri hivyo ni kwamba wakimbiaji wenzangu wengi tuko levo moja tu na mimi, kwa hiyo niliona chochote kinaweza kutokea kwa sababu naamini ni watu ninaolingana nao, namshukuru kocha wangu na Shirikisho la Riadha Tanzania (RT) kwa kuniunga mkono," alisema mwanariadha huyo ambaye mwaka jana alishika nafasi ya nne kwenye mashindano hayo.

Aidha, ameiomba serikali kuusapoti mchezo huo kwa ukaribu kwa sababu, uwezekano wa kufanya vema kwa wanariadha ni mkubwa na nafasi za kufanya hivyo zinaonekana.

Geay ni Mtanzania wa pili kushika nafasi ya pili kwenye michuano hiyo ya 127 tangu kuanzishwa kwake, huku Tanzania ikiweka rekodi ya kushika nafasi ya pili mara nne.

Mwanariadha Juma Ikangaa alishika nafasi ya pili kwenye mbio hizo mara tatu mfululizo, mwaka 1988, 1989 na 1990.




Daktari wa Kamisheni ya Ngumi, Hadija Hamis, akimpima Afya Bondia, James Kiliani jijini Dar es Salaam jana, wakati wa zoezi la upimaji afya kwa mabondia watakaopanda ulingoni kwenye mpambano wa 'Mfalme kwenye Ufalme wake' utakaofanyika mjini Morogoro mwishoni mwa wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kocha wa Ruvu Shooting afungiwa

Na Adam Fungamwango

KOCHA Msaidizi wa Ruvu Shooting, Renatus Shija, amefungiwa kuiongoza timu hiyo kwa mechi tatu na kupigwa faini ya shilingi milioni moja baada ya kuwatolea lugha ya matusi wafanyakazi wa Televisheni ya Azam waliokuwa wanamshawishi akubali kufanya mahojiano.

Kocha huyo pia ametozwa faini ya shilingi milioni moja nyingine kwa kosa lingine la kukataa kufanya mahojiano na mtangazaji wa televisheni ya mdhamini mwenye haki za matangazo.

Adhabu hiyo imetolewa na Kamati ya Usendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), kwenye kikao chake kilichokaa Aprili 15, mwaka huu kupitia mwenendo na matukio mbalimbali ya ligi na kufanya maamuzi hayo.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi, imesema kocha huyo alifanya matukio hayo kwenye mechi ya Ligi Kuu namba 201 iliyochezwa Aprili 9, kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya kati ya Prisons na Ruvu Shooting, wenyeji wakishinda mabao 3-1.

"Kocha Msaidizi wa Klabu ya Ruvu Shooting, Renatus Shija, ametozwa faini ya shilingi milioni moja kwa kosa la kukataa kufanya mahojiano na matangazaji wa televisheni ya mdhamini mwenye haki za matangazo baada ya kumalizika kwa mechi tajwa hapo juu.

"Pia kocha huyo amefungiwa michezo mitatu na kutozwa faini ya shilingi milioni moja kwa kosa la kuwatolewa lugha ya matusi wafanyakazi wa Televisheni ya Azam ambao walikuwa wakijaribu kumsihi akubali kufanya mahojiano," iliandikwa taarifa hiyo na Bodi ya Ligi.

Wakati kocha huyo akifungiwa, Ruvu Shooting ambayo kocha wake mkuu ni Mbwana Makata, iko kwenye hali mbaya katika msimamo wa ligi ikiwa nafasi ya 15 kwa pointi 20, ikisaliwa na mechi nne tu kukamilisha mechi 30 za msimu huu.

# *Pambano la Kiduku 'Mfalme kwenye Ufalme wake' laiva*

Na Saada Akida

HOMA ya pambano la kimataifa kati ya Mtanzania Twaha Kiduku na Iago Kiziria, imeendelea kupanda baada yabondia huyo raia wa Georgia kutarajiwa kutua nchini leo tayari kwa pambano hilo lililopewa jina la Mfalme kwenye Ufalme wake, likitarajiwa kupigwa wikiendi hii mkoani Morogoro.

Kiziria atapanda ulingoni kwenye pambano hilo kuwania mkanda wa Ubingwa wa Universal Boxing Organization (UBO) Inter-Continental dhidi ya Kiduku ambaye atakuwa akitetea ubingwa huo katika mpambano huo utakaopigwa Ukumbi wa Tanzanite mjini Morogoro.

Mratibu wa Habari na Matukio wa waandaji wa pambano hilo, Victor Nyang'amale, wakati zoezi la kupima afya za mabondia lililofanyika Dar es Salaam jana, alisema mpinzani huyo wa Kiduku anatarajiwa kutua nchini leo, Jumatano pamoja na Mtanzania, mwingine anayeishi nchini Ghana, Loren Japhet.

Alisema maandalizi ya pambano hilo yanaendelea vizuri mpaka sasa na wanatarajia kuwapokea mabondia kutoka nje leo tayari kwa safari ya kuelekea Morogoro kwa ajili ya pambano la Mfalme kwenye Ufalme wake.

"Kwanza ni mpinzani wa Kiduku, Iago kutoka Georgia anakuja kuupima ubingwa wa Kiduku ambaye atakuwa anautetea kwa mara nyingine baada ya mwaka jana kumtwanga Alex Kabangu.

"Ukimuondoa huyo, kesho (leo) tunatarajia kumpokea bondia mwingine kutoka Ghana, ni Mtanzania ambaye alihamishia shughuli zake za michezo nchini humo na wengine wanamtambua kwa majina ya Loren Japhet," alisema Victor.

Aliongeza kuwa Loren anarejea nyumbani kupigana baada ya miaka miwili na mara mwisho alimpiga Hamis Morinyo, hivyo anarudi kucheza na Juma Choki katika pambano ambalo kila mmoja anatarajia kuona ngumi za kweli.

"Choki ni mmoja kati ya mabondia wakali, tumeona akipiga mabondia wazuri, tukaona haja ya kuweka hili pambano kwa sababu kwa kipindi kirefu wamekuwa wakikimbiana hivyo Aprili 22 pale Tanzanite, ulingo utakuwa wa moto kabisa, " alisema Victor.

Kwa upande wa daktari wa pambano hilo, Hadija Hamis, alisema imekuwa kawaida kuwapima mabondia afya kabla ya pambano lenyewe kwa lengo la kutimiza kanuni za mchezo huo ambapo jana walipima ugonjwa wa Kisukari, Homa ya Ini, HIV na mimba kwa mabondia wa kike

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICE AITAKA ARSENAL

KIUNGO wa kati wa West Ham na England, Declan Rice, angependelea kuhamia Arsenal katika msimu ujao wa majira ya joto, huku Newcastle pia wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(TalkSPORT)***

### NEWCASTLE YATAKA WANNE

DECLAIN Rice ni miongoni mwa wachezaji Waingereza, ikiwa ni pamoja na kiungo wa Leicester City, James Maddison mwenye miaka 26 na mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney mwenye miaka 27, wanaosakwa na Newcastle United wakitaka kusajili wachezaji wakubwa na wakali wanne msimu huu. ***(Telegraph)***

### GUNDOGAN SAFI BARCA

BARCELONA ina uhakika wa kumsajili kiungo wa kati wa Manchester City na Ujerumani, Ilkay Gundogan, mwenye umri wa miaka 32, kwa uhamisho huru mara tu mkataba wake na timu hiyo ya Ligi Kuu England utakapokamilika msimu wa majira ya joto. ***(Times)***

### SPURS YAMTAKA ENRIQUE

KLABU ya Tottenham Hotspur iko mbioni kuchuana na Chelsea katika mbio za kumwania kocha wa zamani wa Barcelona, Luis Enrique. ***(Telegraph)***

### COTE KUTUA ROMA

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte, huenda akajiunga na AS Roma msimu ujao, huku kocha wa sasa Jose Mourinho huenda akatua Paris Saint-Germain ya Ufaransa. ***(CalcioMercato via Mirror)***

### CORREA ATAKIWA EPL

KLABU za Aston Villa, Everton na West Ham, zote zinavutiwa na mshambuliaji wa Inter Milan mwenye umri wa miaka 28, Joaquin Correa. ***(Sport Witness)***

### GALLAGHER SASA KUUZWA

CHELSEA itajaribu kumuuza Conor Gallagher, 23, msimu huu wa majira ya joto kwenda klabu kadhaa za Ligi Kuu England na Ulaya vinavyomtaka kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 23. ***(Mail)***

### NELSON HATIHATI ARSENAL

ARSENAL imempa Reiss Nelson, 23, mkataba mpya, lakini bado kuna shaka juu ya mustakabali wake wa muda mrefu, huku Aston Villa, Fulham, West Ham na Brighton zikiwa miongoni mwa timu zinazowania kumsajili winga huyo wa England. ***(Mail)***

### MASUAKU KUPIGWA BEI

KLABU ya West Ham inatazamiwa kupokea ada ya takriban pauni milioni 1.75 kutoka kwa Klabu ya Uturuki ya Besiktas kwa ajili ya beki wake wa kushoto wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Arthur Masuaku, 29, baada ya kipengele kwa mujibu wa kumnunua kuafikiwa. ***(Football Insider)***

### WALKER AWINDWA VILLA

ASTON Villa imeweka nia ya kutaka kumnunua beki wa kulia wa Manchester City na England, Kyle Walker, 32, ambaye mkataba wake unamalizika msimu wa majira ya joto wa 2024. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# FAMILIA YA GLAZERS KUBADILI MSIMAMO WA KUIUZA UNITED

**MANCHESTER,** England

**●●● Glazer ambao wanaimiliki klabu hiyo wanazingatia njia mbadala zote za kimkakati...**

JOEL na Avram Glazer wanazidi kujiamini kupata uwekezaji wa nje ambao utawawezesha kubaki kama wamiliki wa Manchester United na uwezekano wa kuongeza maradufu thamani ya klabu katika muongo mmoja ujao, kwa mujibu wa ESPN.

**Familia ya Glazer, ambayo inamiliki United tangu mwaka 2005, ilitangaza Novemba mwaka jana kuwa inazingatia "njia mbadala zote za kimkakati, ikiwa ni pamoja na uwekezaji mpya katika klabu, mauzo, au miamala mingine," ili kuzalisha fedha zinazohitajika kubadilisha timu, mafunzo na Uwanja wa Old Trafford.**

Uwanja huo ulipuuzwa kuwapo kama sehemu ya kwenye mpango wa England na Ireland kuwasilisha ombi la kuandaa Euro 2028 licha ya kuwa mkubwa kwa Klabu za EPL.

Wakati mfanyabishara wa benki, Sheikh Jassim bin Hamad al Thani kutoka Qatar akiwasilisha ombi la kutaka kuinunua United pamoja na bilionea Jim Ratcliffe, tajiri mkubwa wa England, baadhi ya fedha za mwekezaji mwenye makao yake makuu nchini Marekani wamewasiliana na Raine Group, benki ya New York inayosimamia mchakato huo kusajili nia yao ya kupata hisa za wachache katika klabu.

Elliot Investment Management, Ares Management Corporation, Sixth Street Partners na The Carlyle Group zote zinajaribu kupata hisa kwenye klabu ya United, baada ya kuwasilisha nia yao kwa Raine Group kabla ya tarehe ya mwisho ya Aprili 28, mwaka huu kwa zabuni ya tatu.

Wakati mashabiki wa United, ambao wamekuwa wakiwapinga Glazers tangu kuinyakua kwao miaka 18 iliyopita, wameweka wazi kupitia makundi ya mashabiki kuwa wanataka Glazers kuuza hisa zao zote katika klabu hiyo na kuwafungulia njia wamiliki wapya.

Lakini tarifa ya iliyoipata ESPN ni kwamba ndugu Joel na Avram -- wenyeviti-wenza wa United -- wanapendelea uwekezaji mpya ambao utawawezesha kubaki madarakani hapo Old Trafford, pamoja na ndugu na wakurugenzi wenza Kevin, Bryan na Edward Glazer na Darcie Glazer. Kassewitz wakiondoa hisa zao katika klabu.

ESPN iliripoti mnamo Februari kwamba wanunuzi wa United walikuwa na mashaka na nia ya Glazers ya kuuza kabisa klabu hiyo na kwamba Joel na Avram walikuwa na mpango wa kuendelea kushikilia.

Na licha ya zabuni zilizothibitishwa kutoka kwa Sheikh Jassim na Ratcliffe, kupitia kundi lake la INEOS, chanzo kiliiambia ESPN kwamba Joel na Avram Glazer wanaamini kwamba uwezekano wa ukuaji wa klabu katika miaka ijayo unaweza kuifanya United kuwa na thamani ya angalau pauni bilioni 10.

Huku maeneo ya ukuaji yakitarajiwa katika suala la mapato ya matangazo, fursa za utiririshaji na uwezekano wa urekebishaji wa mchezo wa klabu, kuna maoni ndani ya uongozi wa United kwamba klabu inaweza kuwa ya thamani zaidi kwa uwekezaji unaohitajika ndani na nje ya uwanja.

HABARI MICHEZO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,104,5

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 19,20 NA 21 APRILI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/04/23 | 17:00 | Istanbulspor vs Antalyaspor | 2.73 | 3.31 | 2.40 |
| 02. 19/04/23 | 17:00 | Kayserispor vs Kasimpasa | 2.31 | 3.35 | 2.83 |
| 03. 19/04/23 | 18:00 | Fotbal Trinec vs Pribram | 2.68 | 3.09 | 2.42 |
| 04. 19/04/23 | 20:30 | Konyaspor vs Adana Demirspor | 2.61 | 3.30 | 2.51 |
| 05. 19/04/23 | 21:45 | Blackburn vs Coventry | 2.30 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 19/04/23 | 21:45 | Swansea vs Preston | 2.44 | 3.16 | 2.76 |
| 07. 19/04/23 | 22:00 | Bayern Munchen vs Manchester City | 2.54 | 3.41 | 2.48 |
| 08. 20/04/23 | 20:30 | Sivasspor vs Trabzonspor | 2.61 | 3.30 | 2.51 |
| 09. 20/04/23 | 22:00 | Sporting Lisbon vs Juventus | 2.34 | 3.17 | 2.97 |
| 10. 21/04/23 | 01:00 | San Lorenzo vs Fortaleza CE | 2.21 | 3.17 | 3.43 |
| 11. 21/04/23 | 05:00 | Universitario vs Goias | 2.23 | 3.12 | 3.01 |
| 12. 21/04/23 | 05:00 | Deportes Tolima vs CA Tigre | 2.27 | 3.28 | 3.17 |
| 13. 21/04/23 | 19:00 | Apollon Limassol vs Pafos FC | 2.44 | 3.27 | 2.74 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# SERGI AIPA PIGO BARCA

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wamethibitisha kuwa Sergi Roberto, anakabiliwa na kipindi kirefu cha kukaa nje ya dimba kutokana na jeraha la misuli ya paja.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alibadilishwa na Eric Garcia dakika 15 tu baada ya sare ya bila kufungana ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, dhidi ya Getafe baada ya kuuumia mguu wake wa kushoto.


Sergi alifanyiwa uchunguzi juzi Jumatatu na Barca ikaweka wazi kuwa ameumia vibaya kwenye misuli yake ya paja.

Kumpoteza nyota huyo ni pigo kwa klabu hiyo kwani Jumapili wiki hii wanakabiliwa na mchezo dhidi ya Atletico Madrid walio nafasi ya tatu.

Kulikuwa na habari njema kwa wababe hao wa Katalunya kwamba, Ousmane Dembele, Pedri na Frenkie de Jong waliweza kushiriki katika mazoezi.

Xavi alisikitikia hali ya Uwanja wa Coliseum Alfonso Perez baada ya timu yake kushindwa kufunga bao kwenye mechi ya tatu mfululizo.

'The Blaugrana' hao wapo mbele kwa pointi 11 dhidi ya wapinzani wao, Real Madrid wakiwa wamesalia na mechi tisa.



# Klopp: Tumecheza mchezo bora

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amepongeza "mchezo bora zaidi wa Liverpool kwa muda mrefu" baada ya 'Wekundu' hao kuwalaza Leeds United kwa 6-1 katika mechi ya Ligi Kuu England juzi, Jumatatu.

Mohamed Salah na Diogo Jota kila mmoja alifunga mabao mawili, huku Cody Gakpo na Darwin Nunez kila mmoja akifunga moja moja pake kwenye Uwanja wa Elland Road.

Ushindi huo ulihitimisha msururu wa mechi tano bila kushinda kwa Liverpool katika mashindano yote, huku vijana hao wa Klopp wakisonga mbele kwa pointi sita za kufuzu kucheza Ligi ya Europa, wakiwa bado na mchezo mkononi dhidi ya Tottenham wanaoshika nafasi ya tano.

Kocha wa Liverpool alibainisha ukali wa timu yake kama sababu kuu ya kuzuia hali yao mbaya ya hapo awali.

"Nadhani ni mchezo bora ambao tumecheza msimu huu kutoka kwa mitazamo na nyanja tofauti za mchezo," alisema Klopp akiiambia Sky Sports.

"Nadhani tulilazimish makosa mengi, lakini u kuwa mchezo mzuri san mabao ya kustaajabish na upinzani - ulikuv mchezo bora kwa muc mrefu."

Klopp alifafanua zai akipendekeza Liverpo wameanza kurudi kw nye ubora tena katil wakati muhimu.

Aliongeza: "Ni jambo jumla. Ili kucheza mpi mzuri unahitaji utuliv utulivu unaopatikana katika kulinda, lakini u apokuwa katika aina h ya mtiririko mbaya ba unafanya maamuzi yasiy sahihi.

80,144/-

# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/04.23 | 17:00 | Brentford FC vs Aston Villa | 2.41 | 3.20 | 2.75 |
| 02. 22/04.23 | 17:00 | Leicester City vs Wolverhampton Wanderers | 2.38 | 3.15 | 2.85 |
| 03. 22/04.23 | 19:30 | Preston North End vs Blackburn Rovers | 2.46 | 3.20 | 2.70 |
| 04. 22/04.23 | 21:00 | FC Groningen vs NEC Nijmegen | 2.75 | 3.15 | 2.44 |
| 05. 22/04.23 | 21:45 | Sampdoria Genoa vs Spezia Calcio | 2.46 | 3.10 | 2.75 |
| 06. 23/04.23 | 10:00 | Kawasaki Frontale vs Urawa Red Diamonds | 2.37 | 3.10 | 2.55 |
| 07. 23/04.23 | 13:30 | Kasimpasa Istanbul vs Konyaspor | 2.47 | 3.25 | 2.35 |
| 08. 23/04.23 | 15:30 | PSV Eindhoven vs Ajax Amsterdam | 2.32 | 3.40 | 2.75 |
| 09. 23/04.23 | 16:00 | AFC Bournemouth vs West Ham United | 2.85 | 3.15 | 2.39 |
| 10. 23/04.23 | 16:00 | AC Ajaccio vs Stade Brest 29 | 2.95 | 3.00 | 2.42 |
| 11. 23/04.23 | 18:05 | Montpellier HSC vs Stade Rennes | 2.95 | 3.30 | 2.24 |
| 12. 23/04.23 | 18:30 | Brighton & Hove Albion vs Manchester United | 2.32 | 3.45 | 2.70 |
| 13. 23/04.23 | 18:30 | Bayer Leverkusen vs RB Leipzig | 2.55 | 3.40 | 2.49 |
| 14. 23/04.23 | 20:30 | Borussia Monchengladbach vs Union Berlin | 2.28 | 3.20 | 2.95 |
| 15. 23/04.23 | 21:45 | Juventus Turin vs SSC Napoli | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 16. 23/04.23 | 21:45 | Olympique Lyon vs Olympique Marseille | 2.37 | 3.45 | 2.65 |
| 17. 23/04.23 | 22:00 | Sevilla FC vs Villarreal CF | 2.85 | 3.25 | 2.34 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 19/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1641 | FC Ingulets vs Rukh Vinnyky | 2.38 | 2.98 | 2.83 |
| 13:00 | 2212 | Jubilo Iwata vs Yokohama F Marinos | 4.76 | 3.99 | 1.56 |
| 13:00 | 2342 | Kawasaki Frontale vs Shimizu S Pulse | 1.65 | 3.79 | 4.36 |
| 13:00 | 3117 | FC Tokyo vs Gamba Osaka | 2.18 | 3.20 | 3.05 |
| 13:00 | 3817 | Yokohama vs Nagoya Grampus | 4.16 | 3.33 | 1.79 |
| 13:00 | 4309 | Gimpo Citizen vs Busan I Park | 2.89 | 2.99 | 2.33 |
| 13:00 | 4618 | Kashiwa Reysol vs Niigata Albirex | 2.43 | 3.07 | 2.76 |
| 13:00 | 4627 | Sanfrecce Hiroshima vs Vissel Kobe | 1.84 | 3.37 | 3.83 |
| 13:00 | 5283 | Cerezo Osaka vs Kyoto Sanga | 1.76 | 3.42 | 4.15 |
| 13:30 | 2473 | Sangju Sangmu vs Jeonnam Dragons | 1.91 | 3.29 | 3.54 |
| 13:30 | 2825 | Urawa Red Diamonds vs Shonan Bellmare | 1.83 | 3.47 | 3.79 |
| 13:30 | 4754 | Cheonan City FC vs Ansan Greeners | 2.83 | 3.19 | 2.26 |
| 15:00 | 1220 | Arba Minch Kenema vs Ethiopia Bunna SC | 2.61 | 2.82 | 2.76 |
| 16:00 | 1768 | Kairat Almaty vs Akzhaiyk Uralsk | 1.46 | 3.65 | 5.60 |
| 16:00 | 2551 | Fotbal Trinec vs Pribram | 2.66 | 3.22 | 2.36 |
| 16:00 | 3072 | Tobol Kostanay vs Aksu | 1.66 | 3.36 | 4.96 |
| 16:15 | 2632 | Sabah vs Kelantan FA | 1.27 | 4.80 | 7.20 |
| 16:30 | 4196 | Akron Tolyatti vs Spartak Moscow | 5.39 | 3.94 | 1.51 |
| 17:00 | 1533 | Perak FA vs Negeri Sembilan | 5.03 | 3.75 | 1.55 |
| 17:00 | 2466 | Istanbulspor vs Antalyaspor | 3.04 | 3.36 | 2.18 |
| 17:00 | 2908 | Kayserispor vs Kasimpasa | 2.29 | 3.46 | 2.78 |
| 17:00 | 5751 | Pdrm vs Johor Darul Takzim | 15.40 | 6.98 | 1.11 |
| 18:00 | 1847 | Legetafo Legedadi vs Bahir Dar Kenema FC | 9.09 | 4.65 | 1.29 |
| 18:00 | 3120 | Slavia Prague B vs Graffin Vlasim | 2.34 | 3.24 | 2.68 |
| 18:00 | 4380 | HJK Helsinki vs VPS Vaasa | 1.38 | 4.20 | 6.76 |
| 18:00 | 4942 | Neman Grodno vs BATE Borisov | 2.64 | 3.10 | 2.51 |
| 18:00 | 5180 | MFK Karvina vs MFK Chrudim | 1.81 | 3.48 | 3.69 |
| 19:00 | 3858 | Jelgava vs FK Auda | 3.90 | 3.64 | 1.76 |
| 19:00 | 3992 | CSKA Moscow vs Ural Yekaterinburg | 1.62 | 3.59 | 4.89 |
| 19:00 | 5234 | FC Krasnodar vs Kryliya Sovetov | 1.86 | 3.37 | 3.78 |
| 19:30 | 4104 | Lillestrom vs Stromsgodset | 1.62 | 3.93 | 4.72 |
| 19:45 | 4731 | GO Ahead Eagles vs Waalwick | 2.00 | 3.44 | 3.35 |
| 20:30 | 3281 | Konyaspor vs Adana Demirspor | 2.38 | 3.36 | 2.73 |
| 20:30 | 4205 | Basaksehir vs Fenerbahce | 3.68 | 3.58 | 1.87 |
| 21:00 | 4537 | Al Wasl Dubai vs Baniyas | 1.53 | 4.01 | 4.83 |
| 21:00 | 5052 | Ittihad Kalba vs Ajman Club | 2.09 | 3.45 | 2.93 |
| 21:00 | 5784 | Al Ain vs Al Sharjah SC | 2.07 | 3.41 | 2.99 |
| 21:45 | 1403 | Swansea vs Preston | 2.13 | 3.30 | 3.15 |
| 21:45 | 1596 | Blackburn vs Coventry | 2.37 | 3.20 | 2.80 |
| 21:45 | 2274 | QPR vs Norwich City | 3.00 | 3.30 | 2.20 |
| 21:45 | 2672 | AL Markhiya vs Al-Shamal | 2.15 | 3.18 | 3.03 |
| 21:45 | 4297 | Watford vs Cardiff | 1.92 | 3.31 | 3.76 |
| 22:00 | 1736 | Inter vs Benfica | 2.09 | 3.35 | 3.20 |
| 22:00 | 3443 | Middlesbrough vs Hull City | 1.44 | 4.39 | 5.99 |
| 22:00 | 4072 | Bayern Munchen vs Manchester City | 2.54 | 3.52 | 2.42 |
| 22:00 | 4540 | Bogota FC vs Orsomarso | 2.09 | 3.15 | 3.30 |
| 22:00 | 4637 | Reading vs Luton Town | 4.41 | 3.31 | 1.78 |
| 22:15 | 1821 | Farco FC vs Ghazl EL Mahallah | 1.97 | 2.86 | 4.41 |
| 22:15 | 2530 | Talaea El Gaish vs Coca Cola | 4.42 | 2.87 | 1.96 |
| 22:15 | 4555 | National Bank vs Haras EL Hodood | 1.97 | 3.11 | 3.92 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MWANADADA ASHINDA MIL.12/- JACKPOT BONUS YA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

INGAWA ni nadra sana kusikia msichana amebashiri na kushinda, lakini kwa Caroline Kileo hali ni tofauti, kwani yeye ndiye mshindi halali wa Jackpot Bonus ya katikati ya wiki ya mechi 13, akijinyakulia kitita cha Sh. milioni 12.3 baada ya kupatia mechi 12 kati ya 13.

**Caroline anakuwa msichana wa pili kushinda mkwanja mrefu tangu mwaka 2023 ulipoanza, akitanguliwa na Asha Hemed Rajabu, mkazi wa Tandika, Dar es Salaam, ambaye alijishindia Sh, 4,109,805, Januari mwaka huu.**

Akizungumza baada ya uhakiki na makabidhiano ya hundi, Caroline alisema alianza kucheza na SportPesa mwezi mmoja uliopita, baada ya kuona tangazo akiwa anaangalia Star Times TV.

"Unajua mimi nilikuwa nimetulia zangu nyumbani sasa wakati nacheki TV, nakumbuka ilikuwa Star Times tangazo la SportPesa likapita mara ya kwanza, wakati ule sikulitilia maanani, lakini nikakumbuka huwa naona washindi mbalimbali wa SportPesa wakipostiwa mitandaoni.

"Kwa bahati nzuri tangazo lile lilirudiwa tena. Kwenye tangazo kule mwisho wanasema piga *150*87#, nilikuwa na kisimu changu cha kitochi, siku hizi zimezoeleka kama viswaswadu, nikajaribu kufuatisha kama walivyoandika, nikapata sms ikisema karibu SportPesa," alisema Caroline.

Aliongeza kuwa baada ya sms hiyo yalifuata maelezo yaliyokuwa yanashuka chini kwa namba ambapo namba moja ilikuwa michezo ya leo, namba 2 ni beti sasa, namba 3 ni Jackpots, namba 4 ni weka pesa, namba 5 ni akaunti yangu, namba 6 ni toa pesa, 7 matokeo ya mechi na 9 toka.

Baada ya hapo anasema aliuliza kwa watu na marafiki zake wakamuelekeza namna ya kucheza na kiswaswadu, akajaribu akaweza.

"Mimi ni mfanyabiashara wa nafaka niliamua kucheza hizi Jackpots ili nipate mtaji kwa kuwa kila nikiona taarifa kuhusu SportPesa, mara nyingi inahusiana na washindi, hasa hasa hawa wa bonasi, hivyo nilivutiwa kwa kuangalia viwango ambavyo washindi waliotangulia walikuwa wanapata.

"Katika kitu cha ajabu ambacho sijui nilipata wapi msukumo wa namna hiyo, siku naweka mkeka niliweka mikeka saba kwa mpigo, nikijaribisha aina tofauti tofauti za kuweka mikeka. Cha kushangaza, kati ya mikeka saba, mikeka ambayo nilihisi nimetumia akili ndio iliyokufa mapema. Mkeka huu ulioshinda, mimi nilijiwekea mechi bila kuangalia historia wala kuchambua timu au kuzifuatilia. Nilikuwa tu naangalia nabonyeza. wa nyumbani ashinde, au wa ugenini ashinde. Sikutumia kitu chochote ambacho ungeweza kusema kimeniongezea uelewa wa namna ya kucheza, ambacho watu wengi wanaongelea kama uzoefu."

Caroline aliongeza: "Mimi sijui sana mambo ya mipira ila niliamua kuzifukuzia hizi hela za Jackpot, kwa kuwa naona watu wengi wanashinda na kutangazwa katika majukwaa mbalimbali ya habari."

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Kampuni ya SportPesa, Sabrina Msuya, mbali na kumpongeza Caroline kwa ushindi wa Jackpot Bonus ya katikati ya wiki alimtaka kuendelea kucheza Jackpot huenda kuna siku akatimiza ndoto yake ya kuibuka mshindi wa Jackpot yenyewe.




Mshindi wa Jackpot Bonus, Caroline Kileo kutoka Tandika, Dar es Salaam akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 12.3 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13. **MPIGAPICHA WETU**

## Mayele aitoa hofu Yanga kwa Rivers

INATOKA UK. 24

yoyafanya," alisema Harson.

Meneja huyo alisema hana wasiwasi na wapinzani wao hao kwani wamewafuatilia kipindi kirefu katika michezo yao waliyoicheza

Aidha, alisema wachezaji wana morali ya juu kuelekea kwenye mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa.

Kwa upande wa Afisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, ameelezea safari hiyo pamoja na kipigo ambacho timu hiyo ilikipata Jumapili iliyopita dhidi ya watani zao wa jadi Simba, akisema wachezaji wamejisikia vibaya.

Hata hivyo alisema tayari pambano limesha na akili yao sasa ipo kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, pamoja na Kombe la FA.

Kamwe pia aliwasifu wanachama na mashabiki wa Yanga kwa utulivu hata baada ya kupoteza mechi hiyo, akisema ni watu waliokomaa kimichezo.

## VAR kuamua Simba vs Wydad


INATOKA UKURASA 24

ambao wanatarajiwa kutua nchini leo.

"Maofisa wengine wa mchezo huo wakiwamo waamuzi wanatarajiwa kutua nchini kesho (leo), atakayechezesha mchezo huo ni Nouh Bangoura kutoka Senegal , akisaidiwa na Adoh Herman Desire (Ivory Coast) na Maquete Ndiaye (Senegal)," alisema meneja huyo.

Kuhusu wapinzani wao, Wydad, Ahmed alisema wanatarajia kutua nchini leo saa 5:00 asubuhi kwa ndege yao wakiwa na jumla ya watu 50 wakiwamo wachezaji na viongozi wa timu hiyo.

Michezo
Jumatano Aprili 19, 2023
Nipashe



Rais Samia ampongeza Geay UKURASA 20




Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, Allen Mushi (kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 100 kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Imani Kajula, ikiwa ni sehemu ya bonasi ambayo kampuni hiyo inatoa kwa kila hatua ambayo klabu hiyo inafikia kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kuanzia hatua ya makundi. Makabidhiano hayo yalifanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: CARLOS BANDA**

# Mayele aitoa hofu Yanga kwa Rivers

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

HUKU Kikosi cha Yanga kikitarajiwa kuondoka nchini kesho kuelekea nchini Nigeria kwa ajili ya mchezo wao wa mkondo wa kwanza wa robo fainali wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji wao, Rivers United, utakaochezwa Jumapili wiki hii, mshambuliaji wa timu hiyo, Fiston Mayele, amesema wameshasahau matokeo yaliyopita dhidi ya Simba na akili yao ni michuano hiyo ya kimataifa.

Jumapili Yanga ilikubali kipigo cha mabao 2-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya watani wao wa jadi Simba, hiyo ikiwa ni mechi ya mwisho kwao kabla ya kuelekea Nigeria kwenye michuano hiyo ya kimataifa kwa ngazi ya klabu.

Akizungumza na Nipashe jana, Mayele alisema hana shaka na mchezo huo kwani alikuwa anausubiria kwa muda mrefu na matokeo yaliyopita dhidi Simba ameyasahau na Sasa anaelekeza nguvu zake katika mchezo huo.

Kwa upande wa Meneja wa Klabu ya Yanga, Walter Harson, alisema baada ya mchezo wao wa Jumapili waliwapa mapumziko mafupi wachezaji wao na kwamba wataondoka nchini Alhamisi kuelekea Nigeria.

"Timu yetu inatarajia kuondoka Alhamisi kuelekea nchini Nigeria kwa ajili ya mchezo wetu huo, tunaamini tutafanya vizuri kutokana na maandalizi tuli-

INAENDELEA UKURASA 23

# VAR kuamua Simba vs Wydad

## M-Beti yakoleza mzuka, Refa wa kati atoka Senegal kwa kina Sakho, kuziona buku 5, Waarabu kutua leo na...

**Na Saada Akida**

WAKATI Klabu ya Simba ikisema safari hii inahitaji kurudia rekodi ya mwaka 2003 wakati wakimtoa Bingwa Mtetezi wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Zamaleck ya Misri, kwa kumfurumusha nje ya michuano hiyo msimu huu, Wydad Casablanca ya Morocco, mechi hiyo ya robo fainali itaamuliwa na Teknolojia ya Kisasa ya 'Video Assistant Referee', VAR.

**Tayari Kikosi cha Simba kimeingia kambini jana asubuhi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo wa robo fainali dhidi ya Wydad ambao ni mabingwa watetezi wa michuano hiyo, utakaopigwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam majira ya 10:00 alasiri.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema msimu huu wamedhamiria kucheza nusu fainali na wachezaji wanatambua malengo yao hayo kwenye michuano ya kimataifa.

Alisema mechi itachezwa siku yenye baraka ya Eid al-Fitr, hivyo anawakaribisha Watanzania wote kwenda uwanjani kuangalia timu mbili bora zikicheza na Simba ikihitaji kufikia rekodi yao ya kumtoa bingwa mtetezi.

"Lengo letu ni kuwa klabu ya michezo bora barani Afrika, tunaendelea kuboresha hilo kuwa moja ya timu bora 10 Afrika na ndio timu pekee Tanzania ambayo itacheza CAF Super League.

"Tunashukuru wadhamini wetu M-Bet kwa ushirikiano ambao wanatupa, leo watatukabidhi kishika mkono kwa kuingia robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na huku tukitarajia kufanya vizuri mechi ya Jumamosi," alisema Kajula.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema baada ya mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga juzi, Jumapili wachezaji walipewa mapumziko kabla ya kuingia kambini moja kwa moja.

Alisema wachezaji wawili Sadio Kanoute ambaye hakuonekana katika mechi kadhaa zilizopita kutokana na majeraha pamoja na Aishi Manula nao watafanyiwa vipimo.

"Kanoute alipata maumivu ya nyonga na leo (jana) amefanyiwa vipimo kama itaonekana yupo fiti ataanza mazoezi pamoja na wenzake kama ilivyo kwa mlinda mlango Manula, itategemea majibu ya vipimo ili kujua kama wawili hawa watakuwa sehemu ya kikosi.

"Mechi ya Simba na Wydad ndio kubwa barani Afrika wiki hii kwa sababu tunakutana na bingwa mtetezi, lakini pia watu wanataka kuona Mnyama akivunja historia ya mwaka 2003 kwa kumtoa bingwa mtetezi," alisema na kuongeza:

"Wydad tunaenda kumfanyia balaa, hawataamini dhamira yetu, ni kuvunja mwiko wa kuishia robo fainali, kumtoa Wydad tunakiri wametuzidi ubora, lakini tunaimani tunakwenda kuwatoa safari hii tunaitaka nusu fainali."

Aidha, Ahmed alisema tayari tiketi zimeanza kuuzwa na kwamba kiingilio cha chini ni Sh. 5,000 na cha juu kitakuwa ni Sh. 30,000, lakini kutakuwa na vifurushi maalum kama 'Mnyama Package' ambayo ni kwa marafiki.

"Tunazo tiketi za Simba Executive, hii imekuja kwa ajili ya makampuni, taasisi, mashirika kupata tiketi kwa ajili ya wafanyakazi wao, tiketi moja ni Sh. 20,000 na wakinunua watapewa na 'Gate Pass' (kibali) cha kuingiza gari ambalo watalitumia kuja uwanjani.

"Lakini pia tunayo Platinum, hii ni 'special package', ambayo inapatikana kwa Sh. 150,000 kwa ajili ya watu kuja uwanjani kushangilia Simba yao, mpaka jana tulikuwa tumeshaanza kuuza kwa anayehitaji awake oda yake sasa," alisema Ahmed.

Ahmed pia alisema katika mchezo huo, utakuwa na VAR ambapo mwamuzi wake ni Mahmoud Ashoue kutoka Misri akisaidiwa na Djibril Camara kutoka Senegal

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >